SportPesa
TZS. 961,840,460
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 4

**MVUA** kubwa yasababisha vifo watu sita





# Nipashe

Jumamosi Februari 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580868

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


UKURASA 11

## HOFU VITA URUSI

# Serikali yatoa tamko Watanzania Ukraine

**ACT-WAZALENDO** yataka warejeshwe nchini... *Endelea ukurasa 2*



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula

# Mbaroni tuhuma wizi mtandaoni, EFD feki

UKURASA 2



UKURASA WA 3

### WAZIRI ATAKA LUGHA NYEPESI HAMASA CHANJO YA CORONA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy...

UKURASA WA 3

### JAFO ATOA WIKI MBILI MAJITAKA KINONDONI

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo...

UKURASA WA 4

### WALIOPATA MBEGU ZA KAHAWA KUFUATILIWA

NAIBU Waziri Wizara ya Kilimo, Anthony Mavunde, amewataka maofisa ugani mkoa...

## Mwanafunzi aliyeandika barua, arejea shuleni tena

UKURASA 3



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akizungumza na Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa anayeshughulikia masuala ya Amani, Jean-Pierre Lacroix, baada ya kumalizika kwa mkutano wa 10 wa wakuu wa nchi wa Serikali zinazohusika na mpango wa Amani, Usalama na Ushirikiano nchini DRC na kwenye ukanda wa maziwa makuu, jijini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo juzi. **PICHA: OWM**

MICHEZO SIMBA YAANDAA 'SAPRAIZI' UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akimuapisha Kanali Burhan Zuberi Nassor kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Ikulu jijini Zanzibar jana. Habari **Uk. 07. PICHA: IKULU**

# Serikali yatoa tamko Watanzania Ukraine

**Na Maulid Mmbaga**

WIZARA ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imetoa mwongozo kwa Watanzania wanaoishi Ukraine kutokana na hali ya hatari iliyotangazwa huko.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - Wizara ya Mambo ya Nje, Emmanuel Buhohela, Watanzania wanaoishi Ukraine wametakiwa kufuata na kutekeleza maelekezo yote yanayotolewa na Serikali ya Ukraine kwa wasiokuwa raia wa nchi hiyo.

Pia serikali iliwataka kuendelea kuwasiliana na Ubalozi wa Tanzania ulioko Sweden ambao pia unawakilisha Ukraine kwa jambo lolote la dharura kwa kufuata utaratibu wa mawasiliano uliotolewa na ubalozi.

"Wanafunzi wote walioko Ukraine wanatakiwa kufuata maelekezo na miongozo wanayopewa na uongozi wa vyuo vyao, ikiwa ni pamoja na wazazi wa wanafunzi hao kuwasiliana na watoto wao ili kukubaliana utaratibu wa kuwarejesha pale itakapobidi kufanya hivyo," alisema Buhohela.

Aliongeza kuwa hadi wakati anatoa taarifa hiyo jana, hakukuwa na Mtanzania aliyepata madhara yoyote kutokana na hali inayoendelea Ukraine ambayo ilisababisha serikali ya nchi hiyo kutangaza hali ya hatari.

"Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu kuhusu hali za Watanzania walioko Ukraine na inatoa rai kwa wazazi wa wanafunzi wanaosoma nchini humo kuwa watulivu, sambamba na kuwataka Watanzania wote wanaoishi katika nchi hiyo kufuata maelekezo na miongozo inayotolewa na Serikali ya Ukraine," alisisitiza Buhohela.

Wakati serikali ikitoa kauli hiyo, Chama cha ACT-Wazalendo kimetoa rai kwa serikali kuhakikisha Watanzania walioko katika nchi za Ukraine na Urusi wanakuwa salama kipindi hiki cha mgogoro wa kivita ulioanza kuleta madhara kwa binadamu na mali.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana na Naibu Msemaji wa Kisekta wa Mambo ya Nje wa chama hicho, Dahlia Hassan, ni jukumu la serikali kulinda raia na kuhakikisha usalama wao mahali popote.

Hali ya hatari nchini humo juzi iliibuka baada ya majeshi ya Urusi kuanza kuishambulia Ukraine na kusababisha baadhi ya wananchi kuamua kuhama kwa kukimbilia maeneo yenye usalama.

Hassan alisema kuwa hadi jana mchana kulikuwa na vifo 137 na majeruhi 316 vilivyoripotiwa.

"Jambo hilo linatia shaka na wasiwasi mkubwa juu ya usalama wa Watanzania walioko huko. Kutokana na hali ilivyo Ukraine, siyo sawa kwa serikali kuachia jukumu la usalama wa Watanzania mikononi mwa ubalozi peke yao," alisema.

Hassan alisema kuwa kutokana na tukio hilo walitarajia kuona juhudi za dharura na za makusudi za serikali kuwaondoa raia wake Ukraine na Urusi katika maeneo yenye hatari ya vita bila kuchelewa.

Chama hicho pia kilipendekeza hatua tatu za tahadhari zichukuliwe na serikali ili kuhakikisha usalama wa Watanzania walioko katika nchi hizo.

Hassan alisema kwa wakati huu ni vyema serikali ikatuma ndege kwa ajili ya kuwaondoa raia wake kabla hali ya vita haijapamba moto. Hata hivyo, tayari serikali ya Ukraine imeshatangaza kufunga mipaka yake.

Hatua ya pili, alisema: "Kama suala la kuchukua raia wa Tanzania kwa ndege ni gumu kwa wakati huu kutokana na hali ya hatari iliyopo, ni vyema jitihada zifanywe kwa kuondoa Watanzania wote waishio katika miji ya mipakani au wote waishio Ukraine kuwasogeza katika miji inayopakana na nchi jirani kama Poland au kuwasaidia kuwaingiza Poland na nchi zingine jirani zinazopokea watu kutoka Ukraine kwa ajili ya hifadhi na usalama katika kipindi hiki," alisema.

# Mbaroni tuhuma wizi mtandaoni, EFD feki

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa 12 wanaodaiwa kukutwa na mashine ya EFD, nyaraka zenye taarifa za mawakala wa Tigo na za wateja wa benki ya CRDB, ambazo huzitumia kuwaibia wananchi na mawakala fedha zao kwa njia ya mtandao.

Kutokana na kukamatwa kwa watuhumiwa hao, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, jana aliwataka wananchi na mawakala walioibiwa kwa njia ya mtandao, wafike Kituo cha Polisi Oysterbay ambako upelelezi dhidi ya watuhumiwa hao unaendelea.

Alitaja vitu vingine wanavyodaiwa kukutwa navyo ni simu za mkononi 42, kadi za Tigo 55, kompyuta mali ya Tigo na nyaraka za Tigo zikiwa na jumla ya kurasa 1,500. "Vielelezo hivyo walikuwa wakivitumia kufanyia wizi kupitia kwa mawakala na mteja mmoja mmoja kwa kuwapigia simu na kuwatumia ujumbe wakijifanya wafanyakazi wa kampuni za simu, halafu hutoa maelezo ambayo mteja au wakala huwatumia fedha," alisema. Kamanda Muliro alisema wakati mwingine wamekuwa wakitoa maelekezo kwa kujifanya wanahuisha mfumo wa kampuni hivyo wanawatajia wateja na mwisho huwaeleza waweke namba za siri na kuibiwa fedha kwenye akaunti zao.

"Tunawataka watu wote walioibiwa kwa njia ya mfumo huu wafike Kituo cha Polisi Oysterbay, ambako upelelezi dhidi ya watu hawa unaendelea, ili taratibu za kisheria zikamilike wafikishwe mahakamani," alisema. Wakati huo, Kamanda Muliro alisema wanamshikilia Hajji Musa (30), mkazi wa Chamazi, Temeke kwa tuhuma za kumshambulia kwa fimbo na kumsababishia maumivu makali mtoto wake wa kambo mwenye umri wa miaka 11 (jina linahifadhiwa) kwa tuhuma za kuiba Sh. 195,000.

Alisema baba huyo alimtuhumu mtoto huyo kuwa ameiba fedha hizo usiku wa Februari 22 mwaka huu na siku iliyofuata alipokwenda shuleni alidondoka na kupoteza fahamu na kwa sasa anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH). "Uchunguzi wa awali unaonyesha chanzo cha mtoto huyo kuumwa ni kipigo alichopata kutoka kwa baba yake wa kambo. Mtuhumiwa atafikishwa mahakamani," alisema.

Kamanda Muliro pia alisema wanamshikilia mwanaume jina wakilihifadhi kwa tuhuma za kukutwa na magari mawili ya wizi aina ya Toyota Land Cruiser Had Top na Toyota Land Cruiser LX mali ya Dk. Danstan Kabelwa, yaliyoibwa mwaka huu kati ya Januari 7 na Februari 13 eneo la Yombo Vituka, Temeke.

# Mvua yaua watu sita

**Na Hamida Kamchalla,**
TANGA

WATU sita wamefariki dunia mkoani Tanga kutokana na mvua inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini.

Jana Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Msaidizi Safia Jongo, alisema watu hao walifariki dunia kwa nyakati tofauti katika muda usiozidi mwezi mmoja.

"Hii mvua imeacha kilio kwa wananchi wa Tanga kuanzia kipindi cha Januari 11 hadi Februari 22, mwaka huu.

"Katika mvua hii inayoendelea hapa Mkoa wa Tanga, tumekumbana na maafa mbalimbali ikiwamo watu kufa maji. Mpaka sasa, watu sita wamefariki dunia," alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Jongo, walipoteza maisha wanatoka wilaya za Korogwe, Lushoto, Muheza, Handeni na Kilindi.

Alifafanua kuwa katika matukio hayo kulikuwa na watoto wawili, akitoa wito kwa wananchi katika kipindi hiki cha mabadiliko ya hali ya hewa kuchukua tahadhari kwa walioko katika maeneo yenye mito na madimbwi.

"Kipindi hiki cha mvua watu wachukue tahadhari, yale madimbwi waliyozoea siyo yale tena, sasa hivi kina cha maji kimeongezeka.

"Kwa hiyo wasiogelee kabisa kwenye madimbwi wala hiyo mito, lakini pia tahadhari kwa watoto wanapotoka wajulikane wanakwenda wapi kwa sababu wanapoenda sana kucheza kwenye madimbwi, tumepoteza watoto wawili kwenye maafa haya.

"Wananchi wachukue tahadhari hasa wale wanaoishi sehemu za mabonde, mvua inaendelea kunyesha. Ili isiendelee kuleta madhara niwasihi wananchi kufuatilia taarifa mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) kwa kuwa wengi wao hawazingatii na kuchukua tahadhari pindi taarifa hizo zinapotolewa," alihitimisha.

HABARI KITAIFA

# Jafo atoa wiki mbili majitaka Kinondoni

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ametoa siku 14 kwa uongozi kwa Wilaya ya Kinondoni kuhakikisha unatatua tatizo la mfumo wa majitaka katika Mtaa wa Ufipa mkoani Dar es Salaam.

Dk. Jafo alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika Mtaa wa Ufipa na kujionea uharibifu mkubwa wa mazingira utokanao na mfumo wa majitaka ambao miundombinu yake imeharibika na kutiririsha maji taka katika makazi ya watu.

Akiwa katika eneo hilo, waziri huyo alisikitishwa na maelezo ya wataalamu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Wakala wa Barabara Mijini na Vijiji (TARURA) na Manispaa ya Kinondoni kutokuwa na habari kuhusu kero hiyo inayowakabili wakazi wa eneo la Ufipa.

"Wataalamu msikae ofisini tu, tokeni mje msikilize na kutatua kero za wananchi, haiwezekani mimi Waziri wa Mazingira nitoke Dodoma kuja kukagua na kuleta ufumbuzi wa tatizo hili wakati ninyi mpo hapa kila siku," Dk. Jafo alisisitiza.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, alisema atahakikisha tatizo hilo linapatiwa ufumbuzi ndani ya siku 14 kama ilivyoelekezwa na waziri huyo. "Waziri nikuhakikishie sisi Wilaya ya Kinondoni kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi siku ya Jumatatu yaani Februari 28 tutawasilisha kwako mpango kazi wa utekelezaji katika kutatua suala hili," Gondwe alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi wa eneo hilo, Rajab Juma, alisema kero hiyo ya majitaka katika makazi yao ni ya muda mrefu na imekuwa tatizo kubwa hususan kipindi cha mvua ambapo majitaka hufurika na kuhatarisha usalama wa maisha yao.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo (kulia), akimsikiliza Rajab Juma Mkazi wa Mtaa wa Ufipa, Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, wakati akieleza changamoto wanayoipata katika makazi yao kutokana na mfumo wa majitaka usio rafiki kwa mazingira, alipofanya ziara jana. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe. **PICHA: OMR**

# Waziri ataka lugha nyepesi hamasa chanjo ya corona

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amesema bado kuna wananchi wengi hawajapata elimu ya kutosha ya chanjo ya UVIKO-19 na masuala mengine ya afya hususani watoto wa kike na wanawake.

Kutokana na hali hiyo, amekitaka Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA) kuielimisha jamii kwa lugha nyepesi zaidi ya wataalamu wa maendeleo na ustawi wa jamii ili kuondokana na dhana potofu zinazosababisha kutokuwapo na mwamko katika suala hilo.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 19 wa chama hicho unaoongozwa na kauli mbiu 'Kuimarisha Uchanjaji wa Chanjo dhidi ya UVIKO-19 Miongoni mwa Madaktari Wanawake Tanzania'. Alisema MEWATA wanapaswa kujikita kwenye utoaji elimu kwa wananchi kuhusu chanjo ya UVIKO-19 na masuala mengine ya afya na mila potofu za jamii zinazosababisha athari kwa wanawake na watoto.

"Zipo mila nyingi ambazo unakuta mtoto ameng'olewa meno eti kwa sababu alikuwa na homa, vinahusishwa na masuala ya kuota meno kwamba ndiyo yana matatizo, lakini tunazo mila nyingine zinaathiri viungo vya watoto wa kike mfano ukeketaji," alifafanua.

Dk. Gwajima aliwataka watumie nafasi zao kama wataalamu wanawake kuwa mabalozi wazuri kwa kuwafikisha elimu ambao hawajafikiwa ili wafanye uamuzi sahihi wa kujikinga na Uviko-19.

"Wana MEWATA ushirikiano na wataalamu wa ustawi wa jamii utawezesha kuipatia jamii huduma za kisaikolojia pale wanapokumbana na matatizo mbalimbali za kiafya au taharuki za milipuko ya magonjwa kama ilivyotokea wakati UVIKO-19,"alisema.

Waziri huyo alisema wataalamu wa ustawi wa jamii hufikia makundi mbalimbali wakishirikiana na timu za wataalamu wa afya zilizoundwa katika ngazi ya taifa hadi mikoa na kusaidia jamii kuondokana na hali ya hofu kuhusu ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na chanjo.

# Aliyeandika barua arejea shuleni tena

Abdallah Khamis, MTWARA

MWANAFUNZI wa kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Msimbati mkoani Mtwara (jina tunalihifadhi), aliyeripotiwa kuandika barua kwa Mkuu wa Shule hiyo, akieleza dhamira ya kuacha shule, amekubali kuendelea na masomo baada ya wadau kumsaidia kupata vifaa vya shule.

Akizungumza na Nipashe shuleni huko jana akiwa amekabidhiwa madaftari, begi, viatu, mashati mawili ya shule na kitambaa kwa ajili ya suruali za shule, mwanafunzi huyo alisema uamuzi wake wa awali ulitokana na wazazi wake kushindwa kumkamilishia vifaa vya msingi kwa ajili ya masomo.

"Kwanza, ninaomba Watanzania wanisamehe, wazazi wanisamehe, walimu wanisamehe na wakazi wote wa Kata ya Msimbati wanisamehe.

"Ni changamoto za ukosefu wa viatu na uhaba wa chakula nyumbani pale ninapotoka shule ndiyo vilinifanya nichukue uamuzi huo," alisema mwanafunzi huyo.

Aliongeza kuwa kabla ya kuchukua uamuzi huo, aliwauliza wazazi wake uwezekano wa kupata vifaa vya shule pamoja na uhakika wa chakula atakaporudi nyumbani na walimweleza kuwa uhakika wa vifaa hawana na chakula kuna wakati atapata na zipo siku atakosa.

Alisema katika mazingira hayo aliona hataweza kuendelea na masomo na badala yake akafikiria aache shule ili kuwasaidia wazazi wake kuongeza kipato kwa kufanya shughuli ndogo.

"Nilijua wazi kitu ninachofanya hakina faida taifa kwa wazazi na taifa kwa ujumla lakini sikuwa na namna nadhani pia nilizongwa na hasira na nilipanga niondoke niende Kilwa kwa dada yangu ili nikafanye kazi ya uvuvi katika eneo hilo," alisema.

Aliongeza kuwa baadhi ya ndugu zake walimwahidi kumpatia vifaa mwakani, jambo alilodai lilimkwaza kufikia ndoto yake ya kuwa rubani.

Mama Mzazi wa kijana huyo, Salma Mayelo, alisema siku mwanawe alipopeleka barua ya kuacha shule alikuwa anawaandalia chakula na baada ya muda akaambiwa na mwanafunzi mwingine kuwa mwanawe kaamua kuacha shule.

"Mimi nilikuwa ndani na siku aliyopeleka barua sikujua kwani hali yetu ni ngumu na muda wote tunahangaika kutafuta riziki ya kuwasaidia watoto wetu," alisema Salma.

Alisema familia yao ina watoto sita na kijana huyo mwenye ndoto za kuwa rubani, ni mtoto wao wa mwisho.

Mkuu wa Shule ya Msimbati, Hamis Sadala, alisema kuwa baada ya taarifa na sababu za mwanafunzi huyo kuacha shule kuenea, wadau mbalimbali walimpigia simu kwa ajili ya kumsaidia kwa miaka yote minne akiwa shuleni hapo.

"Barua ya mwanafunzi nilipata Februari 22 na Februari 23 nikaingia kwenye kikao kazi ndipo nikatoa taarifa, inawezekana nimeharibu sifa ya mkoa wangu kwa upande mmoja kwa ajili ya taarifa hii ambayo sikuipitisha kwa viongozi wa ngazi zingine lakini pia taarifa imesaidia kijana kupata msaada," alisema Sadala.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kulia), akizungumza katika kikao kazi cha Menejimenti, Wakurugenzi Wasaidizi na Makamishna wa Ardhi wa mikoa, jijini Arusha jana. Wa (pili kushoto) ni Naibu Waziri wa Ardhi, Ridhiwani Kikwete. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

## UKOSEFU WA MAJI

# Kinamama walia kubakwa

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANAWAKE wa vijiji vya Buchambi na Buganika wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wamesema ukosefu wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo yao imesababisha kufanyiwa vitendo vya ukatili njiani wanapokwenda vijiji jirani kuifuata.

Wanakijiji hao waliwasilisha kilio chao hicho juzi katika mkutano wa hadhara wa ulagbishi ulioandaliwa na Shirika la Agape na Her Dignity.

Buchambi na Buganika ni miongoni mwa vijiji ambavyo vinazunguka mgodi wa madini ya almasi wa Mwadui ambao kila mwaka huwa wanapewa fedha kwa ajili ya kutekeleza vipaumbele vyao ikiwamo huduma hiyo ya maji.

Agnes Charles kutoka Kijiji cha Buchambi, alisema wanapofuata maji katika kijiji jirani cha Songwa kwenye bwawa la maji, hukutana na wanaume misituni ambao huwabaka.

Agnes alisema ukosefu wa huduma ya maji safi na salama kijijini huko umekuwa tatizo kwao na watoto wao.

"Watoto wetu wanapotoka shuleni na kufuata maji kwenye bwala la Songwa au Mhumbu hukumbana na madhila ya kubakwa njiani na kusababisha mimba za utotoni," Agnes alilalamika.

Gigwa Bundala, mkazi mwingine wa eneo hilo, alisema wanapochelewa nyumbani kutokana na kufuata maji umbali mrefu, huambulia vipigo kutoka kwa waume zao wakiwatuhumu wametoka kwa 'michepuko'.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Buchambi, Said Mabala, alisema kwenye vijiji vyote ambavyo vinazungukwa na mgodi wa Mwadui huwa wanatoa mapendekezo yao na mwaka jana waliomba kujengewa ofisi ya kijiji na kuwaeleza kwa mwaka huu inabidi waombe huduma ya maji.

Mratibu wa miradi kutoka Shirika la Agape, Peter Amani aliwashauri wanakijiji hao wanapotoa mapendekezo yao kwa mgodi huo, wapitishe vipaumbele ambavyo ni muhimu kwao ikiwamo maji, afya na elimu.

Ofisa Uhusiano kutoka Mgodi wa Mwadui, Hilda Hizza alibainisha kuwa wamekuwa wakitoa huduma kwa jamii kulingana na mapendekezo ya wananchi.

"Kuna vijiji viliomba huduma ya maji vikapewa, ninawashauri katika vipaumbele vya mwaka huu muombe maji, " alisema.

# Waliopata mbegu za kahawa kufuatiliwa

**Na Mwandishi Wetu,** KYERWA

NAIBU Waziri Wizara ya Kilimo, Anthony Mavunde, amewataka maofisa ugani mkoa wa Kagera kuwafuatilia na kuwasimamia kwa kila hatua wakulima wa kahawa ambao watagawiwa bure miche bora ya zao hilo.

Mavunde aliyasema hayo jana alipozindua rasmi mchakato wa kugawa bure miche bora ya kahawa aina ya Robusta kwa wakulima uliofanyika katika Kitongoji cha Karenge, Kijiji cha Kamukwanzi 'B', Tarafa ya Kaisho wilayani Kyerwa mkoani Kagera.

Alisema nia ni kuhakikisha kusudio la serikali la kuzalisha tani 300,000 za kahawa kwa mwaka linatimia ifikapo 2025 na ndiyo maana imegharamia miche hiyo kwa ajili ya wakulima.

Mavunde aliwataka maofisa hao wawatembelee wakulima kila wakati na kutoa elimu kwao kuhusu matumizi ya mbegu bora za kahawa na faida zake ili waachane na ile ya zamani iliyopandwa miaka 25 iliyopita ambayo uzalishaji wake ni wa kiwango cha chini.

"Ninakabidhi hii miche milioni mbili ambayo imegharamiwa na serikali, miche hii imezalishwa na kampuni ya JJAD Kagera Farmers kwa kushirikiana na Bodi ya Kahawa (TCB).

"Kuigawa bure haitoshi kama wakulima hawana elimu na usimamizi wa kutosha, ndiyo maana tunazidi kuboresha huduma za ugani ili kuhakikisha wakulima wanaongeza uzalishaji katika eneo dogo," alisema.

Mavunde alisema serikali imepanga kununua pikipiki ili kuhakikisha maofisa ugani wanawafikia wakulima kwa wakati na upo mpango wa kuongeza idadi yao ambao kwa sasa wapo 6,704 huku wanaohitajika ni 20,000.

Kiongozi huyo aliitaka TCB kutafuta masoko ya kutosha ya zao hilo na kueleza kuwa serikali haitavumilia ucheleweshwaji wa malipo ya wakulima.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya JJAD, Dk. Albert Katagira, alisema fedha za kuzalisha miche hiyo zimelipwa na serikali. Dk. Katagira alisema makubaliano na serikali ilikuwa izalishe miche milioni mbili lakini wamevuka lengo la kuizalisha milioni tatu.

Alisema kuwa ugawaji huo ni wa awamu ya pili na alimwomba Naibu Waziri huyo kuangalia namna ya kuongeza bei ya mche mmoja wa kahawa ambayo kwa sasa ni Sh. 150, lengo likiwa ni kuiwesha kampuni hiyo kuzalisha miche mingi zaidi.

"Kampuni ipo tayari kuzalisha miche hata milioni 10, tunaomba bei ya mche iongezwe," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Primus Kimaryo, alisema miche hiyo milioni mbili iko tayari kugawiwa bure kwa wananchi wa Wilaya ya Kyerwa na maeneo mengine mkoani humo.

"Miche igawiwe kwa wakulima ambao wako tayari wamekwishaandaa mashamba yao kwa ajili ya kupanda hii itasaidia wakulima ambao ni wahitaji kuipata kwa wakati na kupanda kuliko itolewe kwa mtu ambaye hata shamba halijaandaliwa," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Rashid Mwaimu, alitumia fursa hiyo kuwaonya baadhi ya watu wanaokwenda nje ya nchi kufanya biashara ya magendo ya kahawa kuwa watakaokamatwa watachukuliwa hatua.

# Waziri awabana makamishna mkakati Ardhi

**Na Munir Shemweta,** ARUSHA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka makamishna wasaidizi wa ardhi wa mikoa nchini kuwajibika na kutumia wajibu wao katika kutekeleza mikakati ya wizara kufikia malengo.

Pia amewataka makamishna hao kuwapangia majukumu kwa malengo maofisa walio chini yao na kufuatilia kazi wanazowapa mara kwa mara.

Dk. Mabula alitoa maagizo hayo jana jijini hapa wakati akifungua kikao kazi cha Menejimenti na Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa Mikoa kilichofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha.

"Yapo malalamiko ya lugha zisizofaa kwa wateja, hii haikubaliki, fuatilieni hili na kulikemea vikali na kuzingatia misingi na kanuni za utumishi wa umma katika majukumu yenu ya kila siku," aliagiza.

Dk. Mabula pia aliwataka katika utekelezaji mpango mkakati wa wizara, wazingatie vipaumbele vya serikali hususan maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali kupitia kodi ya pango la ardhi.

Akizungumzia makusanyo ya Kodi ya Pango la Ardhi, waziri huyo aliwataka makamishna wa ardhi wasaidizi wa mikoa kuwa wabunifu katika njia za kukusanya mapato.

"'Suala la mtandao kutopatikana muda mwingi linaonekana kuwa kikwazo katika ukusanyaji maduhuli, lifanyieni kazi," aliagiza.

Waziri Mabula pia alihimiza kuongezwa kwa kasi ya umilikishaji ardhi kwa wananchi na kuwataka makamishna hao na wakuu wa idara kuweka malengo kwa kila ofisa mwenye taaluma ya ardhi kuandaa hati.

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, alisema kuwa baada ya kuteuliwa katika nafasi hiyo, alizuru katika baadhi ya mikoa na kubaini shida kadhaa alizozitaja kuwa ni pamoja na kutofikiwa malengo ya ukusanyaji kodi ya ardhi pamoja na baadhi ya halmashauri kutohudumia idara za ardhi kwa madai ya idara hizo kuhamishiwa wizarani.

"Nimeanza kuchukua hatua ili kutatua changamoto hizo ambapo tayari nimetoa maagizo mbalimbali kwenye mikoa na menejimenti ya wizara na ni matarajio yangu kikao kazi hiki kutaibua suluhisho la changamoto hizo," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kijazi, Wizara ya Ardhi imekuwa ikinyooshewa vidole na wananchi kwa masuala ya ukiukwaji wa haki za wananchi na kuchafua taswira ya Wizara na kutaka watendaji wa sekta ya ardhi kujitafakari na kujisahihisha kwa kutimiza wajibu ili kuondoa dhana hiyo.

Aligusia pia mpango wa urasimishaji makazi holela na kueleza kuwa ni matarajio yake kupitia kikao hicho, washirika wake wataibuka na mkakati wa uelekeo wa wizara katika kupanga miji sambamba na usimamizi wa fedha Sh. bilioni 50 zilizotolewa kwa ajili ya mpango wa kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, maarufu KKK.




Wauzaji wa mahindi ya kuchoma wakiendelea na shughuli hiyo kando ya Barabara ya Bagamoyo, eneo la Mbezi Shule, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana, licha ya kuwapo bango lenye ujumbe unaozuia kufanya biashara eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wataka misitu itumike kwa malisho wakati wa ukame

**Na Neema Hussein,** KATAVI

WATAALAMU wa mifugo na uvivu kutoka Nyanda za Nyanda za Juu Kusini na Magharibi wameiomba serikali kuruhusu maeneo ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) yatumike kulisha mifugo kipindi kigumu cha malisho.

Daktari wa Mifugo kutoka Mkoa wa Mbeya, Samora Mshang'a, alitoa ombi hilo jana wakati akiwasilisha matatizo yanayowakabili wataalamu hao katika kikao cha siku mbili kilichofanyika katika Ukumbi wa Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi.

Maombi hayo yalitolewa mbele ya Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Tixon Nzunda, wataalamu hao pia wakishauri wizara iwe inafanya rejea ya mara kwa mara kuhusu bei elekezi ya uuzaji wa mifugo ili iendane na ya soko la dunia.

Wataalamu hao walisema mifugo inahitaji chakula na kuna wakati maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho yanaishiwa chakula licha ya wafugaji kuyaendeleza kwa kupanda malisho.

"Kutokana na tukio lililotokea mwaka jana la ukame inabidi tuangalie maeneo mengine ikiwamo misitu kama itawezekana. Pia tuna tatizo la chanjo za mifugo, bei yake bado iko juu, tunaomba wizara iliangalie hili hasa tukiangalia chanjo ya kichaa cha mbwa," aliomba.

Katibu Mkuu huyo aliwaeleza kuwa suala kuruhusu mifugo kuingizwa kwenye maeneo ya hifadhi kwa ajili ya marisho haliwezi kuwa jambo la kujivunia na suluhisho la kudumu ni kuwa na mashamba kwa ajili ya wafugaji.

Alisema hawawezi kujenga sehemu moja na nyingine wabomoe kwa sababu nchi inaongozwa na katiba, sheria, kanuni na taratibu ambazo zinatakiwa kufuatwa.

Nzunda alisema wanataka kuhakikisha mifugo yote inatambuliwa na inaingizwa kwenye mfumo, akisisitiza kuwa hilo litasaidia kutambua idadi yake na kurahisisha namna ya kuihudumia.

"Utambuzi wa mifugo siyo siasa, ni jambo la kiutendaji, duniani kote suala la utambuzi ni lazima na faida zake zinajulikana. Masuala ambayo ni ya msingi hayawezi kuwa ya kujadiliana kwa karne hii na yeyote anayetuchelewesha hatutamwacha," alionya.

Alisema kuwa vyama vya wafugaji, watendaji wa sekta ya mifugo, viongozi wa mamlaka za serikali za mitaa na mikoa lazima wahakikishe jambo hilo la utambuzi wa mifugo linafanyika kwa weledi ikiwamo kulipa msukumo wa kipekee.

# Wakazi Mbagala kupata mwendokasi mwakani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI wa Mbagala mkoani Dar es Salaam wanatarajia kuondokana na kero ya usafiri ifikapo Machi 2023 utakapoanza usafiri wa mabasi ya mwendokasi.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Kibaha jana, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dk. Edwin Mhede, alisema kwa sasa mradi wa ujenzi umefikia asilimia 44.4.

Alisema kwa mujibu wa mkataba wa mkandarasi, mradi huo utakamilika mwishoni mwa mwezi Machi mwakani na wanapopokea barabara, watakuwa wanakabidhi mtoa huduma wa mabasi yaendayo haraka.

"Licha ya mafanikio na vikwazo ambavyo vilikuwa vinaonekana kwenye sekta yetu ya usafirishaji, Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia taasisi za CBE, SIDO na kitengo chake cha Kaizen, imeona itushirikishe ione iliyofanya kwenye viwanda kama yanaweza kuleta tija na kwenye sekta yetu," alisema. "Katika mafunzo ambayo tumeyapata, tunahitaji kuwa na mabadiliko ya kifikra baina yetu DART na UDART, tumekubaliana kufanya maboresho kwenye huduma zetu kuondoa karaha kwa wateja wetu wakiwamo wa ruti za Kibaha na maeneo mengine," alisema. Mtendaji Mkuu huyo alieleza kuwa wanatarajia kuondoa vikwazo kwa wakazi wa Kibaha kwenye uhitaji wa magari ya moja kwa moja kutoka Kibaha hadi Kariakoo.

Kwa mujibu wa DK. Mhede serikali iko mbioni kuboresha miundombinu ya usafiri ya mabasi yaendayo haraka kwa upande wa Kibaha na maeneo mengine ambayo mabasi hayo yameanza kutoa huduma.

Msimamizi wa Kitengo cha Kaizen kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Jane Lyatuu, alisema mafunzo yanayotolewa na kitengo hicho kwa watendaji wa Sekta ya Usafirishaji, wakiwamo DART na UDART, yametolewa kwa wiki saba na yatakuwa endelevu.

Meneja Upangaji Ratiba na Udhibiti UDART, Daniel Madili, alisema kupitia mafunzo hayo wanakwenda kufanya maboresho kwenye huduma zao kwa wananchi.

## Polisi wapewa mbinu za kukabili uhalifu mtandaoni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, amelitaka Jeshi la Polisi kuendelea kujifunza kwa kina namna ya kukabiliana na uhalifu wa mitandaoni kwa ajili ya usalama wa nchi.

Dk. Yonazi aliyasema hayo jana jijini hapa alipofunga mkutano wa usalama mtandaoni kwa ajili ya jeshi hilo na kamati ya wataalamu ambayo yanahusu upelelezi wa makosa ya kimtandao.

Alisema bado kuna kazi kubwa ya kukabiliana na uhalifu huo kwa kuwa kila siku zinaibuka mbinu mpya za kihalifu.

"Mafunzo haya ni muhimu kwa usalama wa nchi, wizara inaendelea kutenga fedha za kuhakikisha nchi ipo salama," alisema.

Aliongeza: "Katika kujenga uwezo wa nchi, mzigo wa usalama wa nchi tumetwishwa sisi tulio hapa, tuna jukumu kubwa sana kuhakikisha kwamba tunalinda usalama wa nchi yetu kupitia uwezo tuliojengewa."

Dk. Yonazi alisema mafunzo hayo yametolewa na wataalamu wabobezi nchini.

Awali Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Camilius Wambura, alisema jeshi hilo kupitia idara ya upelelezi ambao ndiyo wadau wakuu katika kukabiliana na uhalifu wa mitandao, limezingatia mafunzo hayo kwa umuhimu mkubwa.

"Ni ukweli usiopingika kuwa makosa ya mtandaoni yamekuwa tishio kwa ulimwengu wa sasa, kwa kuwa wahalifu wamehamia huku, kwa kuwa hawahitaji nguvu wala gharama ya kusafiri kutenda uhalifu isipokuwa wanahitaji kutumia akili na vifaa vinavyofanikisha uhalifu huo," alisema.

Alibainisha kuwa maarifa na uzoefu walioupata utasaidia kwa kiwango kikubwa majukumu yao akihimiza kufanya kazi kwa ushirikiano na weledi kwa kuwa kuna wapelelezi wachache ambao sio waaminifu wanachafua taswira ya kazi hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Lala salama Ligi Kuu Bara iwe ya kutorudia makosa

**MZUNGUKO** wa pili au hatua ya lala salama ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2021/2022 ulianza rasmi jana kwa mechi moja kuchezwa kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu mkoani Geita kwa wenyeji Geita Gold FC kuwakaribisha Namungo kutoka mkoani Lindi.

Kuanza kwa hatua hii ni dalili kwamba Ligi Kuu Tanzania Bara inaelekea ukingoni kwa sababu imeingia kwenye duru la mwisho ambalo linatoa bingwa na timu zitakazoshuka daraja kuelekea Ligi ya Championship nazo zitajulikana.

Katika kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri, timu , waamuzi na viongozi kila mmoja anatakiwa kutimiza vyema majukumu yake kwa ajili ya kufanikisha klabu anayoitumikia iweze kufikia malengo iliyojiwekea wakati msimu huu unaanza. Nipashe inaamini kila timu wakati inafanya mchakato wa usajili wa wachezaji pamoja na kuajiri benchi la ufundi, iliweka mipango na malengo yake ya nini inahitaji kukipata ndani ya msimu huu na utekelezaji wake ulianzia hapo na si vinginevyo.

Hatuamini kama kuna timu ilianza msimu bila ya kuweka malengo, na kama ipo, basi haistahili kuendelea kuwapo kwenye ligi hiyo ya juu ambayo hutoa mwakilishi au wawakilishi wa nchi kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo hufanyika kila mwaka.

Timu iliyojiwekea malengo yake, inatakiwa kuendelea kutembelea ndoto hizo kwa sababu bado mechi zilizobakia ni nyingi na endapo wachezaji wake watapambana na kucheza soka la kiwango cha juu basi kuzifikia itakuwa ni jambo linalowezekana na kamwe haipaswi kukata tamaa.

Tunaamini kila timu inaweza kufikia malengo yake kwa sababu mpira wa miguu ni mchezo wa makosa, hivyo timu ikijipanga sawa sawa na kutumia vyema mapungufu ya klabu pinzani, tunahakika mwisho wa msimu itakuwa na kicheko na wale ambao wataendelea kuwa wasindikizaji, watavuna walichokipanda.

Weledi huu wa viongozi, wachezaji na waamuzi pia unazihusu timu zinazoshiriki Ligi ya Championship (zamani Ligi Daraja la Kwanza) na First League (zamani Ligi Daraja la Pili), ambazo zinaendelea kwenye viwanja mbalimbali nchini, tena michezo yake ikionekana kuwa na ushindani, pengine kuliko baadhi ya mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Juhudi na maarifa yakifanyika vyema, basi kila timu itafikia malengo yake na kwa kuamini muda wa kurekebisha makosa bado upo, wale waliofanya vizuri katika mzunguko wa kwanza wanaweza kuharibikiwa na timu zilizojifunza kupitia makosa yao, zinaweza kuibuka na kukaa kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hizo na kujiepusha na majanga ya kushuka daraja. Kuna makosa na mapungufu mbalimbali yalifanyika katika mzunguko wa kwanza na kusababisha baadhi ya timu kuona zinaonewa huku wengine wakifaidika na madhila hayo, tunawakumbusha wote wanaohusika na kusimamia michezo hiyo kufanya kazi kwa weledi ili mwisho wa msimu, nchi ipate bingwa ambaye anastahili kubeba taji hilo.


Huu ni wakati wa waamuzi ambao wamekuwa wakibeba lawama za kupendelea baadhi ya timu kuchezesha mechi zote kwa weledi katika duru hili la lala salama kwa ajili ya faida ya soka la nchi yetu.

Msimu huu umeonekana pia kuna ushindani katika Ligi ya Championship, ambayo hutoa timu zinazopanda daraja kushiriki Ligi Kuu msimu ujao. Kwa maana hiyo, waamuzi na maofisa wote wanaosimamia ligi hii wanatakiwa kufuata vyema kanuni, taratibu na sheria zilizowekwa ili pia kupata bingwa na wawakilishi ambao ni imara watakaopanda daraja na kuhimili ushindani kwenye ngazi inayofuata katika msimu ujao.

Katika kuhakikisha makosa ya waamuzi hayajirudii, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), huandaa semina kabla na katikati ya msimu ili kuwakumbusha waamuzi namna ambavyo wanatakiwa kutekeleza majukumu yao, na hili limefanyika, hivyo wadau wa soka wanatarajia kuona mabadiliko katika uchezeshaji.

Waamuzi wanapofanya majukumu yao vizuri, kamwe hakutakuwa na malalamiko ya aina yoyote kuhusiana na upangaji wa matokeo na mwisho wa msimu timu zitakazostahili kubeba taji la Ligi Kuu, Ligi ya Championship, First League na Ligi ya Wanawake Tanzania ambayo nayo msimu huu imekuwa na mvuto atapatikana na atapigiwa makofi na klabu nyingine walizokuwa wakishindana kuwania ubingwa huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kwa ratiba hii ya Bara, hongereni Bodi ya Ligi



Na Adam Fungamwango

**MARA** baada ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Jumatano iliyopita kwa mechi kati ya Mtibwa Sugar dhidi ya Yanga, iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro, Bodi ya Ligi ilitoa neno.

Bodi ya Ligi ilisema ni jinsi gani ilivyoweza kujidhatiti katika mzunguko wa kwanza na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa hasa eneo la utawala, ufundi na ratiba, huku ikiahidi kulifanyia kazi eneo linalolalamikiwa la waamuzi. Ofisa Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Ligi, Almasi Kasongo, alisema kwa asilimia kubwa mzunguko wa kwanza ulikwenda kama walivyopanga, huku akiahidi kuzifanyia kazi changamoto zilizojitokeza kwa ajili ya kuboresha hatua ya lala salama kwa kuifanya iwe nzuri na wa kuvutia zaidi kuliko hatua ya awali.

"Kiukweli tumekwenda kama tulivyopanga, kalenda imeenda na uhalisia tuliotarajia, kiutawala na kiufundi pia, mzunguko wa pili tutafanya kama tulivyofanya mzunguko wa kwanza na kurekebisha baadhi ya changamoto zilizojitokeza, hasa upande wa baadhi ya waamuzi tunaendelea kulipatia ufumbuzi pia," Alisema Kasongo na kuongeza.

"Siku zote kwenye tamu hakukosi kuwa na chungu, changamoto za baadhi ya waamuzi zilijitokeza, nashukuru hata waandishi walizungumzia katika sura ua kujenga, tutazichukua na kuzifanyia kazi, ili mzunguko wa pili ukianza ibaki kuwa historia na kama zikijitokeza basi ziwe mpya, ambazo ni zenye tija na siyo za kubomoa, kuharinu au kusababisha matukio, na matarajio yetu ni kufanya vizuri zaidi kuliko hata mzunguko wa kwanza," alisema Ofisa Mtendaji Mkuu huyo.

Kwanza kabisa napenda kutoa shukrani kwa Bodi ya Ligi. Pamoja na baadhi ya changamoto zilizopo, lakini sisi tulianza kuangalia au kufuatilia ligi kwa muda mrefu, tunaona kwa misimu hii miwili, na hasa huu, Bodi ya Ligi imejitahidi sana hasa upande wa ratiba.

Baadhi ya mechi ya Mtibwa na Yanga, timu zote 16 zilikuwa zimemaliza mechi za mzunguko wa kwanza, kila timu ikicheza mechi 15.

Cha kufurahisha ni kwamba hata Simba, ambayo iko nchini Morocco kucheza mechi ya kimataifa, iliondoka nyumbani ikiwa imecheza mechi yake ya 15 kabla ya zingine. Wakati zilizobaki Bongo zikimalizia, yenyewe tayari ilishamaliza.

Ni tofauti na zamani, ambapo tulishuhudia vituko. Kuna msimu Yanga ilikuwa inashiriki mechi za kimataifa, ikawa na viporo vinane. Simba nayo ilishawahi kuwa na viporo saba misimu michache iliyopita, kiasi hata iliporejea nchini kwenye mechi za kimataifa, ikawa inachezeshwa Jumanne, Alhamisi, Jumamosi, Jumatatu, Jumatano, ili mradi ilikuwa inapumzika siku moja tu, ili mradi ifukuzane na kalenda ya kumaliza ligi. Si tu kwamba ilikuwa ikizichosha timu hizo, lakini pia hazikutendewa haki, wala kuzitendea haki timu zingine.

Kwenye soka, timu zinapofukuzana kusaka ubingwa, au kupigania kubaki Ligi Kuu moja ikiwa imetangulia mechi tatu au zaidi dhidi mwenzake, hakuna haki inayotendeka hapo.

Huko huko nyuma, ndiko tulikowahi kushuhudia hata mechi ya Ligi Kuu kati ya Ndanda FC dhidi ya Yanga ikichezwa Dar es Salaam, badala ya Mtwara kama kanuni zinavyosema.

Vyovyote baadhi ya wapingaji watakavyosema kama vile ni kwa sababu msimu huu timu nyingi zimetolewa mapema kwenye mechi za kimataifa na imebaki Simba tu, au Ligi Kuu ina timu chache sana ambazo ni 16, tofauti na zamani ambapo kulikuwa na timu 20, lakini ukweli unabaki pale pale tu kuwa Bodi ya Ligi inastahili sifa kwa hili.

Kilichobaki sasa ni kufanyia kazi changamoto zilizobaki kwa baadhi ya waamuzi, lakini si kwa kuwapa presha, au kuzionea timu ndogo na kuzipendelea timu kubwa ili ndiyo waonekane wametenda haki, la hasha. Ni kwamba tu wachezeshe kwa haki, bila kujali makelele ya mashabiki na baadhi ya viongozi wa klabu, ili mradi tu wana uhakika walichofanya ni sahihi. Kwenye uamuzi haiwezekani kila mtu akaridhika. Bodi ya Ligi inafaa ishikilie hapo ilipo hadi ligi itakapomalizika, watu waendelee kusifia na si kusahau kila kitu kizuri kilichofanywa kwenye mzunguko wa kwanza. Ndiyo, binadamu wanaweza kusahau kila kitu, kama kuna mambo ya ajabu yatafanyika kwenye mzunguko wa pili, na kuharibu kila kitu kizuri cha mzunguko wa kwanza.

# ‘Nitakamata mke wangu akiuza dawa za kulevya’

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Hassan Mwinyi amemuapisha Kanali Burhani Zuberi Nassor kuwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, huku kiongozi huyo akisisitiza kuwa yuko tayari kumtia mbaroni hata mkewe akijihusisha na biashara hiyo haramu.

Hafla ya kuapishwa kiongozi huyo ilifanyika Ikulu jijini Zanzibar jana ikihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali akiwamo Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, na Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kula kiapo hicho, Kamishna huyo alisema kupambana na dawa za kulevya ni jambo linalohitaji ushirikiano.

Alisema Serikali ya Zanzibar imechukua sura mpya kulingana na nchi zingine duniani ambazo zimeweka sheria kali na zinazodhibiti dawa za kulevya.

Kamishna huyo aliongeza kuwa sheria iliyopo hivi sasa ni mpya, hivyo inahitaji ushirikiano mkubwa kutoka kwa wananchi pamoja na viongozi kwa kuwa uhalifu bado upo katika jamii hasa ikizingatiwa Zanzibar ni kisiwa na ina bandari bubu zipatazo 371.

“Hii dhima ni kubwa lakini kwa pamoja tutahakikisha kwamba Zanzibar bila ya dawa za kulevya inawezekana na dira ya mamlaka ni kuhakikisha kwamba Zanzibar inakuwa huru kutokana na dawa za kulevya ifikapo mwaka 2050,” alisema Kanal Nassor.

Aliongeza: “Kwa sheria hii mpya hakuna mtu anayeitwa papa na kila mtu yuko chini ya sheria na nitahakikisha hata akiwa mke wangu anashiriki dawa za kulevya, anakamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria, sitokuwa na muhali wala sitomwonea mtu isipokuwa nitatimiza wajibu wangu na matakwa ya sheria hii.”

Alimshukuru Rais Dk. Mwinyi kwa kumhakikishia kumpa ushirikiano mkubwa kwa kumpatia vifaa vya kutosha katika mapambano hayo sambamba na ahadi iliyotolewa na Serikali ya Uingereza baada ya kutia saini makubaliano ikiahidi kuleta vifaa kwa kuunga mkono juhudi hizo ambapo hivi sasa wako katika mchakato wa kuangalia vifaa vinavyohitajika.




Meneja wa Benki ya CRDB Tawi la Palm Beach Primier, Pendo Kitula (kulia), akishirikiana na Balozi wa Biko Kajala Masanja (kushoto), kumkabidhi mshindi wa bahati nasibu ya Biko, Ahmad Ally Mbwana, sh. milioni 10, tawini hapo, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kuibuka mshindi kwenye droo kubwa zinazofanyika kila Jumapili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utegemezi halmashauri bado wa kiwango cha juu

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Prof. Riziki Shemdoe, amesema kwa sasa halmashauri nchini zina uwezo wa kujitegemea kwa wastani wa asilimia 15, huku zikitegemea serikali kuu kwa asilimia 85.

Kutokana na hali hiyo, amezitaka halmashauri kubuni vyanzo mbalimbali visivyoumiza wananchi ili zijitegemee.

Prof. Shemdoe aliyasema hayo jana jijini hapa kwenye mkutano wa programu ya maboresho ya usimamizi wa fedha za umma (PIC) kilichojumuisha makatibu tawala wa mikoa, wataalamu wa utekelezaji wa programu hiyo na wadau kutoka Uingereza, Canada na Norway.

Alisema halmashauri hizo awali zilikuwa na uwezo wa kujitegemea kwa wastani wa asilimia nane, lakini kupitia programu hiyo ambayo imetekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano ambacho kinakoma Juni mwaka huu, uwezo umeongezeka kufikia asilimia 15. “Kuna vitu ambavyo mradi huu umesaidia, ulikuwa ukipata ufadhili kutoka kwa wenzetu Serikali ya Uingereza, lakini pia fedha za ndani ambazo Rais Samia Suluhu Hassan alikubali zitumike kuendeleza kazi hii.

“Vitu tulivyofanikiwa kwenye programu hii ni kuzisaidia halmashauri zote kupandisha ukusanyaji wa mapato.

“Ukiangalia mwaka 2015, ukusanyaji wa mapato umeongezeka japo bado utegemezi wa mamlaka za serikali za mitaa kwa serikali kuu ni mkubwa, lakini kwa namna tunavyokwenda ukichukua takwimu za mwaka 2016, mamlaka za serikali za mitaa zilikuwa na uwezo wa kujitegemea kwa asilimia nane tu, asilimia 92 walikuwa wanategemea kupata ‘support’ (usaidizi) serikali kuu.

“Kwa mradi huu na kwa namna tulivyokuwa tunafanya kazi tukiendelea na programu hii ya maboresho tutafika mahali mamlaka zetu zitajitegemea zenyewe, majiji yamekuwa na uwezo mkubwa zaidi ya hii asilimia 15 hii tumechukua kwa halmashauri zote,” alisema.

Kiongozi huyo alisema programu hiyo imesaidia kupunguza hoja za ukaguzi na kwamba wanajikagua wenyewe.

“Tuone kwenye awamu ya sita ya programu hii mambo yapi yatafanyika, lakini ni pamoja na kwenye maeneo haya niliyotaja ili kuongeza uwezo wa halmashauri na kupunguza matumizi ya fedha mbichi, kuna maeneo hela mbichi ilikuwa inatumika kwa kiwango kikubwa, pia suala la ununuzi lizingatiwe na hii PPRA watatuongoza,” alisema.

# Tanzania yapata upendeleo India

**Na Romana Mallya**

UBALOZI wa India nchini umewataka wafanyabiashara wa Tanzania kuuza na kuongeza biashara zaidi na nchi hiyo kwa sababu bidhaa zao hazina mshindani kwenye soko lao.

Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari na kuongeza kuwa hazina ushindani kwa sababu zinapokewa bila kutozwa ushuru.

Pradhan alisema ni wakati wao kuchangamkia fursa kwa sababu bidhaa za Tanzania zimepata upendeleo maalumu, hazitozwi kodi.

“Mazao ya kilimo kama korosho, mbaazi, kunde, dengu na maparachichi yanaingizwa nchini India bila ushuru, Watanzania mchangamkie fursa hii kuuza mazao haya na mengine ili kukuza ushirikiano wa kiuchumi,” alisisitiza.

Balozi huyo alisema India inatumia mafuta ya karanga, alizeti na matunda kama maembe na kwamba bidhaa hizo zikizalishwa zina soko kubwa na la uhakika na kuwahakikishia wafanyabiashara kuwa milango iko wazi.

Aliongeza kuwa licha ya kuwapo kwa athari za corona, uchumi wa nchi yake unaanza kutengamaa ukikua kwa zaidi ya asilimia 9.5.

Alisema uzalishaji wa chanjo wa kuwachanja wananchi, umefanikiwa jambo linaloleta tumaini jipya kiuchumi.

Alisema India ni mwekezaji mkubwa nchini na kwamba taifa hilo sasa litaongeza uwekezaji kwenye maeneo mapya ya kimkakati, akitaja bahari (uchumi wa bluu), uwekezaji kwenye bandari, elimu, umeme, gesi na mafuta.

“Bahari ya Hindi ni eneo linaloigusa Tanzania na India, linatuunganisha. Tuko upande mwingine na Tanzania upande wa pili, tunakutana pamoja eneo hili, tumeamua tushirikiane pamoja kwenye ulinzi, kutunza bahari na vitega uchumi vingine.

“Ushirikiano huu wa bahari unagusa sekta nyingi kama utalii, uvuvi, viwanda vya kuchakata na kufungasha samaki lakini la muhimu kuimarisha usalama,” alisema.

Balozi Pradhan alisema kwenye eneo la bandari kampuni kubwa za India za usafirishaji na kuhudumia shehena zitawekeza wakati kwenye elimu wanaangalia fursa za kufungua taasisi zaidi za elimu na majadiliano na serikali yanaendelea kufanikisha uwekezaji zaidi.

Akizungumzia masuala ya huduma muhimu za jamii kama maji, alisema Tanzania na India zimeunda kamati ya pamoja ya maji, ambayo nchi yake itaisaidia kuboresha upatikanaji na usambazaji wa maji nchini.

Alisema nchi yake imeisaidia Tanzania kwenye miradi ya maji lakini wataalamu wa India watashirikiana kuwapa mafunzo wataalamu wake kwenye utunzaji wa rasilimali maji (water management) mbinu bora za kusambaza huduma hiyo kwa kila mwananchi na uboreshaji.



Msajili wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Mhandisi Rhoben Nkori akichukua maswali kutoka kwa makandarasi kwenye mafunzo ya siku tatu aliyoyafunga jana. Kulia ni Meneja wa kanda ya kati wa bodi hiyo, Yunus Maonyesho na (wa pili kushoto) ni Mratibu wa Mafunzo wa bodi, Neema Fuime. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Makandarasi 4,000 wafutiwa usajili nchini

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

BODI ya Usajili wa Makandarasi (CRB) imewafutia usajili makandarasi zaidi ya 4,000 kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ubabaishaji kwenye utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Hayo yalibainishwa juzi na Msajili wa Bodi hiyo, Rhoben Nkori, wakati akizungumza kwenye hafla ya kufunga mafunzo ya siku tatu kuhusu usimamizi wa miradi kwa makandarasi wazalendo. Alifafanua kuwa hatua ya kuwafutia usajili huwa ya mwisho kabisa baada ya kuona mkandarasi amekuwa sugu licha ya kuonywa na kurekebishwa mara kwa mara kuhusu mwenendo wake kwenye utekelezaji wa miradi.

"CRB ikiona mwenendo mbaya wa mkandarasi tunamwita na kuzungumza naye kujaribu kumrekebisha lakini ikionekana ameshindikana kabisa, tunamfuta na hawezi tena kufanya kazi za ukandarasi nchini.

"Kuna ambao wanajirekebisha na tukijiridhisha tunampa usajili na anaendelea na kazi lakini akionekana ameshindikana tunamfuta kabisa," alisema.

Katika hatua nyingine, Nkori aliwataka makandarasi hao kusoma mikataba kwa makini kabla ya kutia saini ili wasije kukimbia kazi kwa kubanwa na vifungu vilivyomo kwenye mikataba wanayoingia na wateja wao.

Alisema uzoefu unaonyesha kwamba baadhi ya makandarasi wanapoona fedha nyingi kwenye mikataba wanakimbilia kutia saini bila kujua athari zitakazowakuta iwapo watashindwa kutekeleza yaliyomo kwenye mkataba na wateja wao.

"Kuna mwingine akishasaini mkataba anautupilia mbali lakini niwaambie kila mara unapaswa kuangalia unasemaje, ukikwama kitu, rudi kwenye mkataba angalia athari utakazopata kisha endelea na kazi.

"Wengine mnakimbia kazi na mkikutana na watu mnaogopa mnadhani mnatafutwa na polisi. Ni heri ukae bila kuwa na kazi kwa muda mrefu kuliko kulazimisha kazi ambayo itakufanya kuwa mtumwa.

"Unaonekana uko eneo la kazi lakini unaishi kwa tabu mpaka unahama nyumbani kwako, sasa shida yote hii ya nini?" Nkori alihoji.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Florida Women Empowerment, Theresia Komba, aliomba serikali kuwawezesha makandarasi wanawake ambao bado hawajawa na uzoefu wa kufanya miradi wapewe kama sehemu ya kuwajengea uwezo wa kutekeleza ile mikubwa.

Alisema makandarasi wengi wanawake wanakosa miradi kwa kigezo cha kutokuwa na uzoefu, hivyo wakiwezeshwa kupewa itawajengea uwezo na watapata fursa ya kukua na kuwa na kampuni kubwa.

Komba alisema serikali na taasisi za kifedha zinapaswa kutoa kipaumbele kwa makandarasi wanawake kwa kuwapa mikopo ya kufanyia miradi ya ujenzi wanapokwenda kuomba mikopo.

"Mitaji ni tatizo kwa makandarasi wanawake lakini kama taasisi za fedha zikitupa kipaumbele na kutupa mikopo kila tunapopata kazi, tunaweza kufanya mambo makubwa na uzoefu tutapata kama tutakuwa na miradi ya kufanya," alisema.

# DAS ahimiza watumishi kutatua kero za wananchi

**Na Happy Severine,** MASWA

KATIBU Tawala Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Agnes Alex, amewataka viongozi waliopewa dhamana ya kuwatumikia wananchi, wafanye hivyo ili kukidhi matarajio yao.

Akizindua kikao cha uraghbishi jana mjini Maswa, Agnes alisema wananchi wana matarajio makubwa kutoka kwa viongozi wao na endapo hawatawatumikia ipasavyo, dhana ya kuwa na maendeleo shirikishi itakuwa ndoto kwao.

Alisema takwimu za Shirika la Twaweza kuhusu ushirikiano wa viongozi na wananchi zitasaidia kuyashughulikia matatizo yanayokabili wananchi wilayani humo.

Akiwasilisha taarifa ya shughuli za uraghbishi wilayani humo, Ofisa Mwandamizi kutoka Shirika la Twaweza, Richard Temu, alisema utafiti wao umebaini wananchi hawahudhurii mikutano ya vijiji kwa sababu haizungumzii vipaumbele vyao badala yake viongozi huenda na ajenda zao.

Diwani wa Ng'wigwa wilayani humo, Steven Dwese, alikiri kuwa wakati mwingine wakiitisha mikutano ya kijiji, wananchi hawajitokezi kwa sababu ya mgongano wa kisiasa kwenye maeneo yao.

Meneja Programu wa Shirika la KASODEFO, Marius Isavika, alisema kuwa baada ya shughuli za uraghbishi kumekuwapo na hamasa kubwa kwa viongozi na wananchi kushiriki mikutano ya hadhara kwa ajili ya kujadili shughuli za maendeleo yao.

# The Global Fund kupewa ushirikiano

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kuendeleza ushirikiano kati yake na Mfuko wa Kimataifa wa Kusaidia Mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (The Global Fund) katika kuhakikisha afya za wananchi zinaimarika na kufanya shughuli zao katika mazingira salama.

Mkurugenzi wa Idara ya Sera na Uratibu wa Shughuli za Serikali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, Paul Sangawe, aliyasema hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na wadau hao jijini Dodoma.

Sangawe alisema lengo la kukutana kwao ni kuweka mikakati thabiti ya kuimarisha mapambano dhidi ya magonjwa hayo pamoja na kufanya mazungumzo na viongozi wa wizara na taasisi zinazotekeleza miradi inayofadhiliwa na mfuko huo.

Alisema ipo haja ya kusimamia vyema misaada inayotolewa kwa manufaa ya taifa.

"Tumejadiliana pia kuhakikisha tunaelekeza fedha zote za miradi kila baada ya miaka mitatu na kuangalia uwekezano wa kuzalisha baadhi ya vifaa tendanishi ambavyo kwa sasa vinaagizwa kutoka nje.

"Kwa hiyo tutaangalia kwa namna gani misaada inayotolewa inatumika kwa ufanisi na kuleta tija kwa taifa siyo tu kuzalishwa ndani pia kutoa ajira," Sangawe alisema.

Mkuu wa Idara ya Afrika wa Global Fund, Linden Morrison, alishukuru serikali kwa jitihada zake za kuhakikisha wanapambana na magonjwa mbalimbali ili wananchi wake kuwa na afya bora.

"Serikali ya Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika mapambano ya magonjwa mbalimbali kwa sababu wananchi hawawezi kufanya shughuli za uzalishaji kama hawana afya bora na katika hili Global Fund tuko tayari kushirikiana na Tanzania," Morisson aliahidi.

Viongozi na wadau hao wamekutana na Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ina wajibu wa uratibu wa utekelezaji wa programu ya Global Fund na shirika muhimu linaloleta tija katika utekelezaji wa miradi.

Jukumu lingine la ofisi hiyo ni kufuatilia fedha zote zinazotolewa na wafadhili na kuhakikisha zinatumika kama ilivyokusudiwa pamoja na kuhimiza wadau kuzitumia kwa wakati.



# Watumishi wamlalamikia DED madai lugha chafu

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

BAADHI ya watumishi wa Halmashauri ya Kondoa Mji mkoani Dodoma wamemlalamikia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Paul Sweya, wakidai kuwanyanyasa ikiwamo kutumia lugha za matusi dhidi yao.

Kilio cha watumishi hao kilitolewa jana katika mkutano wa kazi baina ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, watumishi wa halmashauri hiyo, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wakuu wa taasisi.

Akitoa malalamiko hayo kwa mkuu wa mkoa, Ofisa Ugavi wa Halmashauri hiyo, Ramadhan Fabian, alidai mkurugenzi wao amekuwa akiwafanyia mambo ambayo yanawavunja moyo kujitoa kufanya kazi.

"Ndugu mkuu wa mkoa, ninashukuru sana kwa ujio wako. Sisi Kondoa hapa kuna shida kubwa sana lakini watu wanakaa kimya tu kwa kuogopa lakini mimi leo nitasema ukweli. Mkurugenzi wetu anatunyanyasa sana, inafikia hatua anatutukana hadi matusi ya nguoni, mimi na utu uzima wangu.

"Muda mwingi tunatumia hadi mishahara yetu kufanya mambo ya maendeleo ya halmashauri yetu lakini hatambui umuhimu wetu. Mimi nimechoka, natamani kuondoka hata leo na wewe. Siwezi tena kuendelea kuvumilia kubaki hapa, ninataka kuondoka hata sasa hivi," alilalamika.

Alidai kuwa kutokana na hali ya manyanyaso hayo, wakuu wa Idara mbalimbali katika halmashauri hiyo wameshindwa kutoa mawazo yao ili kuleta tija katika mambo mbalimbali ya maendeleo.

"Mkuu hawa watu wa CMT hapa wanaumwa ila wanajifanya hawataki kuongea kweli, kukaa kimyaa ni busara lakini mimi leo nimeshindwa kuvumilia. Haiwezekani kuendelea kunyanyaswa kwani nimetoka katika mikoa mingine wala sikuwahi kuwa na kashfa hata ya wizi, kwa nini yeye aendelee kutunyanyasa na kutupuuza?" ofisa huyo alihoji.

Alisema kuwa moja ya sababu za halmashauri hiyo kufanya vibaya katika mambo mbalimbali ikiwamo elimu na ukusanyaji mapato, ni uhusiano mbaya uliopo baina yao na mkurugenzi.

"Hapa umeuliza DT (Mweka Hazina) wa halmashauri umeambiwa hayupo lakini ukweli ni kuwa kakimbia kwani hana majibu, hapa kilichopo ni kuna watumishi wa halmashauri na watumishi wa mkurugenzi, hivyo wengine wakieleza jambo wanasikilizwa na sisi tukitoa hata ushauri wa jambo fulani tunapuuzwa.

"Tunamshukuru sana mkuu wa wilaya kwa busara zake lakini asingekuwa yeye angeshatuweka hata ndani mkurugenzi," alilalamika.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mtaka, alimpongeza mtumishi huyo kwa kuwa mkweli badala ya kuendelea kubaki na jambo moyoni. "Siku zote rafiki wa kweli ni yule anayekueleza ukweli mbele ya macho yako na ogopa sana mtu anayezungumza nyuma ya kisogo chako, huo ni unafiki.

"Ili kufanikiwa katika jambo lazima utengeneze timu yako lakini kwa namna hii inaonyesha kabisa Kondoa ipo shida kubwa sana. Kama hamtabadilika, hakuna mtakachokifanya hapa pamoja na udogo wa halmashauri yenu yenye kata nane, mtakuwa wa mwisho kila kitu," alionya.

Baada ya mkutano huo, Mtaka alitembelea Shule ya Sekondari ya Wasichana Kondoa na kuzungumza na wanafunzi walio katika madarasa ya mitihani, akiwasisitiza kusoma kwa bidii. "Kila mwanafunzi aliyekuja shule kaja kwa ajili ya kusoma na siyo jambo jingine, hivyo msome ili mfaulu katika masomo yenu," alisema.

Aliwataka walimu kuwa wabunifu kwa kuandaa mitihani ya mara kwa mara ya ujirani mwema kati ya shule zilizopo mkoani Dodoma.

"Kwa mwanafunzi wa kidato cha sita atakayepata daraja la kwanza la pointi tatu, mkoa utatoa Sh. milioni moja kwake na kila alama A itanunuliwa kwa Sh. 30,000 na kwa kidato cha nne tutamlipia ada na alama A itanunuliwa Sh. 20,000 sasa kazi ni kwenu someni sana," aliahidi.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Mazingira, Edward Nyamanga (kulia), akiwa katika ziara ya kutembelea Msitu wa Mzakwe- Bonde la Makutupola jijini Dodoma jana, kujionea zoezi la upandaji miti linaloratibiwa na Ofisi yake kwa kushirikiana na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Ofisi za Bonde na JKT Makutupola. Wengine Mkurugenzi wa Mazingira Dk. Andrew Komba (katikati) na Meneja Msaidizi Maendeleo ya Misitu kutoka TFS, Patricia Manonga. **PICHA: ROBERT HOKORO**RO

# TAMISEMI yaonya ukwepaji matumizi mashine za EFD

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imewataka wataalamu wa fedha wa mamlaka za mikoa na serikali za mitaa kuepuka kutotumia mashine za kielektroniki kwenye ukusanyaji wa mapato kwa kuwa ni uvunjifu wa sheria.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - TAMISEMI (Afya), Dk. Grace Magembe, alitoa angalizo hilo juzi jijini hapa kwenye kikao kazi cha Kamati ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Mradi wa Fedha za Umma (PIC) kilichowakutanisha watalaamu wa masuala ya fedha katika ngazi ya Wizara Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wizara ya Fedha, mamlaka za serikali za mitaa na wadau wa maendeleo.

Alisema kutotumia mashine hizo kunaenda kinyume cha malengo ya serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Aliwataka maofisa wasimamizi wa fedha katika mamlaka hizo kuwa na malengo yanayoendana na serikali kwa kutumia mashine hizo kwenye ukusanyaji wa mapato.

Alisema kuwa ili halmashauri zisimame na kujitegemea, ni lazima watalaamu hao wasimamie ukusanyaji wa mapato ya halmshauri kwa kutumia mashine za kielektroniki.

"Usimamizi wa fedha za umma unaendana na uwapo wa maendeleo katika eneo husika, hivyo ni lazima kuzingatia sheria katika ukusanyaji ili wananchi wawe wanufaika wa maendeleo," alisema.

Akizungumzia mradi wa PIC ulivyosaidia kusimamia fedha za umma katika ukusanyaji wa mapato ya mamlaka za mikoa na serikali za mitaa, Naibu Katibu Mkuu huyo alisema zipo halmashauri ambazo vyanzo vya mapato vimeongezeka kutokana na kutumia teknolojia za kisasa ikiwamo mifumo iliyowekwa katika ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za kielektroniki.

# Askofu awaonya vijana kulalamika kukosa ajira

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Kilutheri la Kiinjili (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, amewataka vijana kuacha kubweteka kulalamika hawana ajira, badala yake wajikite kwenye kufanya ujasiriamali ili kujiinua kiuchumi.

Kiongozi huyo wa kiroho aliyasema hayo jana alipofungua Mkutano wa Vijana wa Ushiriki Ujenzi na Utunzaji wa Amani Kupitia Uhusiano wa Kiuchumi na Kitamaduni kwa Maendeleo Endelevu uliofanyika jijini Dodoma ukishirikisha vijana kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alisema vijana wanapaswa kuacha fikra za kukaa vijiweni kupoteza muda kuongea mambo yasiofaa ambayo yanachangia kuwadumaza akili ya kubuni miradi mbalimbali.

Askofu Kinyunyu alisema lengo lao kama viongozi wa dini ni kuona vijana hawaendi kinyume cha maadili ambayo wanafundishwa na wazazi na shuleni, akisisitiza ndio sababu ya kuandaliwa kwa semina kama hiyo ili kuwakumbusha vijana wajibu wao.

"Ninawaomba vijana jengeni tabia ya kujituma na kuacha kukaa vijiweni kujadili masuala yasio na msingi, fanyeni kazi kwa bidii ili kupunguza malalamiko yanayochangia uvunjaji wa amani miongoni mwenu," alisihi.

Askofu huyo alisema wajibu walionao vijana hivi sasa ni kulinda amani iliyopo na kutumia nguvu zao kufanya kazi ambazo zitasaidia kuleta maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

Alisema vijana wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuilinda amani kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuepuka kukaa kujadili mambo yasiofaa ambayo matokeo yake huingia tamaa za kufanya uhalifu.

Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Kamati ya Amani mkoani hapa, Sheikh Kisusu Mwangonga, aliwataka vijana kuwa na sauti moja katika utekelezaji wa maendeleo ili kudumisha amani iliyopo nchini.

Aliwataka kutumia elimu waliyoipata katika semina hiyo kuwafundisha vijana wengine ambao hawajaipata kwa lengo la kujenga nchi na kutunza amani kupitia uhusiano wa kiuchumi.

Sheikh Mwangonga aliwapongeza KKKT kwa kuandaa semina hiyo, huku akiwataka kuandaa kongamano kubwa ambalo litashirikisha vijana wengi zaidi ili kuhakikisha wanapata elimu ya utunzaji amani iliyopo nchini.

Mmoja wa washiriki wa semina hiyo, Samwel Mahazi, alisema vijana hivi sasa wanapaswa kuamka na kutumia teknolojia iliyopo kwa ajili ya kuleta maendeleo katika taifa.

Alisema vijana kwa sasa wana kila sababu ya kubuni vitu mbalimbali vya maendeleo badala ya kubaki nyuma kwa kuwa teknolojia imekua, ikimwezesha mtu kufanya maendeleo hata kupitia simu ya kiganjani.

"Naomba vijana wenzengu tutumie mafunzo haya kama chachu ya kwenda kubadilika katika ufanyaji wa maendeleo, tusitumia teknolojia hiyo kufanya maovu," alisema.





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Muhammed (kulia) akiwa na Mwanasheria Mkuu wa serikali ya Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib, wakifuatilia kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yasema Watanzania walioko Ukraine wako salama

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema suala la mgogoro wa Urusi na Ukraine ni la kidiplomasia na raia wa Tanzania, wakiwamo wanafunzi walioko Ukraine wako salama.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alibainisha hayo alipotoa taarifa ya serikali kuhusu mgogoro wa uvamizi wa Urusi katika nchi jirani ya Ukraine.

Alitoa taarifa hiyo baada ya Mwakilishi wa Mwera, Mihayo Juma Nhunga, kutaka kupata taarifa ya serikali kuhusu mgogoro huo na hali ya wanafunzi wa Tanzania walioko katika vyuo vya nchi hiyo.

Waziri huyo alisema tayari wanafunzi wote wa Tanzania walioko Ukraine wamepewa maelekezo na ubalozi wao ulioko Sweden kuhusu hali halisi ya nchi hiyo huku wakitakiwa kuwa watulivu.

Alisema barua ya nakala hiyo imewasilishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwataka wanafunzi kusubiri maelekezo yote yatakayotolewa na Serikali ya Ukraine. Alisema Serikali ya Ukraine yenyewe imetoa mwongozo kwa wageni wakiwamo wanafunzi wa mataifa mbalimbali ya kigeni wanaosoma katika nchi hiyo wakitakiwa kuwa watulivu.

"Nakala ya barua kutoka kwa ubalozi wetu ulioko Sweden ambao unafanya kazi zake Ukraine umewataka wanafunzi wote wa Tanzania walioko nchi hiyo wawe watulivu huku wakisubiri maelekezo yatakayotolewa na serikali ya nchi hiyo," alisema.

Aliongeza kuwa mipaka yote katika nchi ya Ukraine imefungwa, hivyo hakuna mtu au mwanafunzi anayeweza kupenya na kukimbilia nchi jirani ikiwamo Belarus au Poland. "Leo nimezungumza na kijana wangu anayesoma Ukraine, ameniambia yupo salama na wenzake wote katika makazi yao huku wakisubiri maelekezo ya ziada kutoka kwa Ubalozi wa Tanzania ulioko Sweden," alisema.

Nchi ya Urusi imeivamia Ukraine huku jumuiya za kimataifa zikiitaka Urusi kuondoa majeshi yake haraka.

# Wizara yakumbusha sheria ya kulinda miti

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ya serikali ya Zanzibar, imesema sheria namba 10 ya mwaka 1996 inapiga marufuku ukataji wa miti ambayo ipo katika hifadhi ya taifa ikiwamo mikoko.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Dk. Soud Nahoda, aliyaeleza hayo jana wakati akitoa ufafanuzi kuhusu kasi ya ukataji wa mikoko kwa ajili ya matumizi ya kuni na mkaa katika maeneo ya hifadhi ya taifa.

Alisema sheria hiyo inakataza ukataji wa miti iliyopo katika hifadhi ikiwamo mikoko kutokana na faida zake katika kudhibiti kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya nchi kavu.Waziri huyo alisema kasi ya ukataji wa miti imekuwa ikiongezeka siku hadi siku na kuyataja maeneo ya Chwaka Wilaya ya kati Unguja, Charawe pamoja na kisiwa kidogo cha Uzi kwamba yanaongoza. Alisema katika kisiwa cha Uzi, wananchi wamekuwa wakijipenyeza katika eneo la hifadhi ya miti ya mikoko na kukata miti kwa ajili ya kuni na mkaa.

Waziri huyo alisema Kisiwa cha Pemba ambacho kwa asilimia 70 kimezungukwa na miti aina ya mikoko, kwa sasa kinakabiliwa na kasi ya ukataji miti, hali inayotishia athari za mazingira na maeneo ya Wete, Kengeja na Mjumbini yanaongoza.

"Tutaanza kuzitumia sheria za kulinda mazingira ya hifadhi ya miti ya Mikoko kwa ajili ya kulinda mazingira kwa sababu tumebaini kuna kasi kubwa inayotishia uhai wa miti hiyo Unguja na Pemba," alisema.

Waziri Nahoda alisema wizara yake imeanza kuimarisha vitalu vya miche ya mikoko ambavyo vitasambazwa na kugaiwa bure kwa wananchi wanaoishi maeneo ya ukanda wa baharini.

Alisema wamefanikiwa kuvishawishi vikundi mbalimbali vya uhifadhi wa mazingira kuona kwamba wananchi wanaotesha mikoko kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira.

# Zanzibar kuziimarisha huduma za kisaikolojia

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imeahidi kuendelea kuimarisha nyumba salama za kutoa huduma za kisaikolojia na kijamii, ushauri nasaha na kisheria kwa ajili ya waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Vilevile, imesema haina mpango wa kuwahifadhi kwa muda maalumu wanaume wanaopiga wake zao.

Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazru, alibainisha msimamo huo wa serikali jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kikwajuni, Nassor Salum Ali.

Mwakilishi huyo alitaka kufahamu kama serikali haioni haja ya kuanzisha utaratibu wa kijamii wa kuwahifadhi kwa muda maalumu wanaume wanaowapiga wake zao huku hatua nyingine za kisheria zikiendelea.

Akijibu swali hilo, waziri huyo alisema kwa sasa serikali itaendelea kuwatumia wataalamu wa saikolojia na ushauri nasaha kwa hatua za awali za kuwasaidia wanaume wenye tabia za kuwapiga wake zao ili kuwarejesha katika hali zao za kawaida.

Aliwataka wanaume kuepukana na tabia ya kuwapiga wake zao na kusababisha athari mbalimbali ikiwamo za saikolojia na kifo, badala yake waende sambamba na usemi 'mke hapigwi mateke wala bakora bali hupigwa kwa mvao wa kanga'.

"Hakuna sheria yoyote inayoruhusu wanaume wanaowapiga wake zao kuchapwa viboko hadharani kwa kuwa serikali yetu ni muumini wa kuheshimu haki za binadamu na imeridhia mikataba ya kimataifa mbalimbali ikiwamo Mkataba wa Haki za Binadamu na mikataba mingine," alisema.

Alisema sheria zimetoa mwanya wa kifungo kwa muda maalumu, faini na vifungo vya maisha ikiwa kama sehemu ya kurekebisha jamii kwa wanaume wenye sifa za kufanya matendo kama hayo.



**MARIOO**
UKURASA 12

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI FEBRUARI 26, 2022



# OMBA RADHI
# Diamond ang'ang'aniwa hadharani

SASA ni wazi uongozi wa mwanamuziki mahiri nchini, Diamond Platnumz, wanahangaika kuhakikisha sakata la mwanamuziki huyo kuonekana akiwa na bendera ya kibaguzi linaisha haraka.

Sakata hilo liliibuliwa na mwanamuziki wa Hip hop, Wakazi, ambaye alimshauri Diamond kuondoa kwenye video ya wimbo wake mpya 'Gidi' bendera ya Confederate, ambayo ilitumika katika majimbo ya Marekani yaliyojitenga yaliyokumbatia utumwa wa watu weusi.

Kutokana na ushauri huo, watu wengi wamejitokeza kufafanua suala hilo, lakini wote walifikia muafaka kuwa jambo hilo linawakera watu weusi ambao waliathirika na utumwa nchini humo.

Katika kuonyesha kwamba hata wao wameanza kuwa na hofu, waliomba kama kuna watu wenye maoni ni busara kama wangewapa kwa njia ya siri na sio hadharani.

Kauli hiyo, inaonekana kutompendeza Wakazi, kwani amekataa dhana hiyo akisema kitu kilichokuwa hadharani ni lazima kisemwe mbele ya umma.

Akitolea mifano kadhaa ya wasanii mbalimbali waliofanya makosa na wakasemwa hadharani, hivyo suala hilo ni muhimu kukosoa hadharani.

"Kilio cha baadhi yenu ni kwa nini sijaenda 'Private' kuwaelekeza. Kwamba wafanye kitu hadharani alafu mimi nitoe maoni kwa siri, ikumbukwe kuwa wao sio wa kwanza kufanya makosa ya namna hii, na pia sio wa kwanza kwa sisi kuwasema hadharani tena kwa kushauri na sio kuwazodoa wala kukejeli,"amesema Wakazi.

BASI SAWA

## Yanga Tamu yamnogesha Marioo



WIMBO wa 'Yanga Tamu' ulioimbwa na Marioo, unazidi kukimbiza katika mitandao ya kijamii tangu uzinduliwe mapema wiki hii.

Marioo ambaye amevunja rekodi ya kuhama ushabiki wa timu kubwa za hapa nchini, katika uzinduzi huo alitangaza kurudi tena timu yake ya zamani ya Yanga baada ya kuihama kwa muda akienda Simba mwaka juzi.

Katika mtandao ya You Tube, wimbo huo umetazamwa na watu zaidi ya 500,000 kwa muda wa wiki moja, kitu ambacho ni mwendelezo mzuri wa mwanamuziki huyo.

## Rayvanny hataki ugomvi akiondoka



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Rayvanny, amesema akitaka kuondoka katika lebo ya WCB si suala la ugomvi, kutishana na kuvimbiana.

Amesema ikifika wakati wa kutoka atafanya hivyo, lakini atatumia busara kuwaomba ili kuepusha malumbano na maneno ambayo huwa yanawagombanisha wasanii.

"Bado Wasafi familia yangu nitaendelea kuwa nao, najua binadamu lazima mtakosana lakini haitafika mbali ya kutunishiana misuli," amesema rayvanny.



## Chudy Love asifia 'Utamu' uliomdatisha

MSANII chipikizi wa Singeli, Masoud Ahmad maarufu kama Chudy Love, ameachia kazi yake mpya inayoitwa 'Utamu' ambayo imeanza kuwapagawisha mashabiki wa muziki.

Akizungumza na BT, Chidy Love, amesema wimbo huo ni maalum kwa watu wote wanaofurahia maisha kwa sababu unabeba ujumbe maalum wa upendo.

C hidy Love tayari anatamba na nyimbo zake kali kama Chimamy, tuma,Sawa na Mapenzi Matamu.

"Kitu kiwe kitamu kinabeba nafasi kubwa katika jamii, iwe chakula mapenzi au michezo kinaishi katika jamii kwa muda mrefu," amesema

Amesema wimbo huo ambao umerekodiwa katika studio ya Coll Music, video yake ipo mbioni kukamilika hivi karibuni.

## Zanda: Nusu mrembo, nusu jini

**Na Adam Fungamwango**

'ZANDA' ni filamu inayoonyesha dhana ya kuwepo vitu ambavyo si vya kawaida kwenye dunia hii ya Mungu.

Kuna viumbe ambavyo havionekani kwa macho ya kibinadamu kama vikitaka. Na binadamu anaweza kuwaona kwa muonekano wowote ile kama viumbe hivyo vitahitaji. Anaweza kujigeuza binadamu au mnyama. Hao ni majini, unaweza pia kuwaita mashetani. Hawa mbali na kujigeuza chochote, wana uwezo wa kuingia ndani ya binadamu na kufanya vitu ambavyo unaweza kudhani anayefanya ni yule mnayemfahamu, kumbe ni kiumbe kingine kabisa ambacho kimeingia ndani yake.

Filamu hii imechezwa na Fadhili Msisili, Benadetha Deus, Said Matochi, Mwajuma Issa, Lukya Yahaya na wengineo wengi.

Zanda ni msichana mrembo kwenye himaya ya chifu Msisiri. Lakini ni msichana mwenye kiburi, mvivu na aliyesikia. Anaishi na mama yake tu. Baba yake hajulikani yupo wapi.

Hali hii ilimfanya asiwe na raha na mara kwa mara alikuwa akikwaruzana na mama yake kuhusu hilo. Hali ilivyokuwa mbaya ilibidi mama afunguke

Akamhabarisha kuwa baba yake ni marehemu. Aliuawa na watu wawili wasiokuwa wa kawaida waliowakuta porini wakienda shambani, wakati huo yeye mjamzito.

Baada ya hapo akajifungua mtoto ambaye ndiye Zanda porini na ghafla akajitokeza bibi kizee mchawi, aliyemuonyesha njia akiwa na mtoto mchanga.



Cha ajabu alipomaliza tu mama kumuelezea binti yake hivyo, sura ya Zanda iligeuka na kuwa kama shetani, akamkaba mama yake na kumuua. Baadaye akarudi kwenye hali ya kawaida. Kijiji kizima hakikujua nini kimetokea. Kilidhani tu kuwa alifariki ghalfa akizungumza na binti yake.

Baada ya hapo hali kijijini ikabadilika. Watu wakaanza kuuawa ovyo, wengine kuwa vipofu na wengine waliobahatika kukiona kitu kinachowadhuru walikuwa ni Zanda.

Binti mrembo, akageuka shetani linamaliza watu na kutia wengine vilema kijijini hapo.

Akaogopwa hata na mjomba na shangazi yake wanaomlea. Anaweza kuwa Zanda wa kawaida, lakini haijulikani muda na saa ambayo atageuka na kuua mtu.

Wanakijiji wakaenda kwa Chifu Msisiri ambaye sasa waliamua kwenda kwa mganga Kizalala. Baada ya kuangalia kwa makini akawaambia kuna Zanda wawili, mmoja ni huyu wa kawaida, na mwingine ni jini. Linalowamaliza wanakijiji ni Zanda jini linalomwingia Zanda wa ukweli na kufanya maafa, kisha linatoka na kumwacha mwenyewe.

Haikuwa kazi ndogo. Kazi ilifanyika hadi mganga akafanikiwa kumuua jini Zanda na kumbakisha mwenyewe ambaye ni mpole na mnyenyekevu.





## Monalisa hofu tupu

VITA vilivyoanza kati ya Urusi na Ukraine, umekuwa mwiba mchungu kwa mwigizaji mkongwe, Monalisa, baada ya kuonyesha kuwa na hofu kuhusu usalama wa mtoto wake.

Msanii huyo, kutumia ukurasa wake wa Instagram, ameandika kwamba kuwa mapigano hayo yanampa hofu juu ya usalama wa mwanawe hasa kutokana na kukosekana usafiri wa ndege kutoka Ukraine ambako yuko mtoto wake.

"Tumbo linanicheza kama mzazi, Ukraine hakuna ndege, nampataje mwanangu?...Mungu wasimamie watoto wetu" ameandika Monalisa.

## SOLO 5 KALI ZA HAYATI NENE TCHAKOU

**Na Adam Fungamwango**

"TCHAKOU Tchakou, Tchakou baba, Tchakou baba ooo ooo." Ni utambulisho wa nyimbo nyingi ambazo gita la solo limepigwa na moja kati ya wapigaji wa magitaa hayo ongozi, nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo na Afrika kwa ujumla Nene Tchakou. Anakuwa anatajwa na waimbaji wanaoimba nyimbo ambazo anapiga solo.

Si Watanzania wengi wanaojua kuwa mwanamuziki huyo amefariki dunia. Nene alifariki dunia Januari 28 nchini Marekani alikokuwa akiishi, akiwa na miaka 64.

Mwanamuziki huyo ambaye alijipatia umaarufu Afrika, ikiwemo Tanzania ambako ana mashabiki wengi kutokana na aina yake ya upigaji wa gitaa la solo, kwa miaka minne alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa kupooza.

Jina lake kamili ni Nene Mbendi Mondasa, na alizaliwa Banana Bas Congo mwaka 1957 na alianza muziki mwaka 1973 kwenye bendi ya Bella Negrita na baadaye Minzoto Wella Wella.

Umaarufu wake ulianza alipojiunga na Grand Zaiko Wawa chini ya uongozi wa Felix Manuaku Waku mwaka 1983.

Marehemu alipiga muziki nchi mbalimbali za Ivory Coast na nchini Ufaransa. Watanzania walianza kumfahamu miaka ya 1990, kutokana na kupiga solo kwenye ngoma mbali za wanamuziki, Kanda Bongoman, Yondo Sister, Soukous Stars, huku akipiga gita karibuni nyimbo zote za Allain Kounkou, Nimon Toki Lala na bendi nyingi. Hizi ni baadhi ya nyimbo tu ambazo amepiga sita la solo.

**Isambe Monie-Kanda Bongoman**

Ni wimbo maarufu sana nchini Tanzania kwa mashabiki wa muziki kuanzia miaka ya 1990 na kuendelea. Ulivuma kama moto wa nyika unaowaka kwenye upepo mkali. Isambe ni moja kati ya nyimbo ambazo Nene Tchakou amezitendea haki sana kwenye kuchambulia gitaa, likiwafanya mashabiki 'kuchizika' kwa kucheza, huku mwenye Kanda Bongoman akipagawa na kumwita 'Tchakou Tchakou Tchakou baba, Tachakou baba, ooo ooo. Wimbo huo ndiyo ulibeba jina la albamu iliyotoka mwaka 1990.

**Jo-Yondo Sister**

Kwenye albamu ya mwanamuziki Yondo Sister iitwayo 'Derniere Minute' ya mwaka 1995, Nene alitwanga nyimbo moja iitwayo 'Jo'. Humo alifanya balaa na ni moja ya wimbo wa Yondo uliopendwa sana na Wabongo.

Shimita, ambaye ni mmoja wa waimbaji walioimba wimbo huo, hakuacha kupagawa na kumwita 'Tchakou Tchakou Tchakou baba, aye mabe'.

**Muchana-Kanda Bongoman**

Huu nao ni moja kati ya nyimbo maarufu za mwanamuziki Kanda Bongoman ambazo Nene alipiga solo ya hatari. Ingawa ni wimbo wa taratibu, lakini gitaa lake ni tamu la kubembeleza kiasi kwamba unaweza kusahau shida zako kwa muda ukiusikiliza.

**Je Me Sens Bien-Yondo Sister**

Wimbo huu wa 'Je Me Sens Bien', nao upo kwenye albamu ya 'Derniere Minute' ya Yondo Sister. Jamaa alifanya balaa hadi anaitwa 'Nene Tchakou ale ale chuwaaa'.

**Sana-Kanda Bongoman**

Wimbo 'Sana' una baadhi ya maneno ya kiswahili 'Ninakupenda sasa, ninakupenda wewe'. Wimbo huu pia solo limepigwa na Nene Tchakou. Ni mwanamuziki ambaye atakumbukwa sana kwani aliweza kuchuana na wapiga solo mahiri kama Diblo Dibala, Dally Kimoko, yeye akionekana kufuatia na wengine kama vile Benico Ipopolipo, Saladin Ferreira, Caen Madoka, Syrian Mbenza na wengineo. Buriani Nene Tchakou.






## Zlatan kweli watoto wote wako?

INAWEZEKANA rapa Omoniyi Raphael, maarufu kama Zlatan, amevunja rekodi kwa wanamuziki vijana nchini Nigeria, baada ya kutangaza anatarajia kupata mtoto wake wa kumi hivi karibuni.

Mwanamuziki huyo nyota, ametumia mitandao ya kijamii kuweka tangazo hilo huku akiweka picha ya mtoto wake wa pili akiwa na miaka minane.

Zltan alipata mtoto wake wa kwanzaTolu-walase, miaka kumi iliyopita na kila baada ya mwaka mmoja amekuwa akimtambulisha mtoto wake mwingine.



## Pole Okoye Mungu atakusaidia

MSANII wa muziki kutoka Nigeria, Paul Okoye, ambaye anaunda kundi la PSquare, amejeruhiwa baada ya kufanya onyesho nchini Liberia.

Kupitia video iliyosambaa katika mitandao ya kijamii, anaonekana mwanamuziki huyo akiwa amelala sakafuni huku mguu wake mmoja ukivuja damu.

Mwanamuziki pacha,Peter Okoye na wachezaji wao pia walionekana kuchanganyikiwa kutokana na tukio hilo.

## Kifo cha Ricky pasua kichwa

BADO kuna utata kujua chanzo kilichosababisha kifo cha mwanamuziki maarufu wa Hip hop nchini Afrika Kusini, Ricky Rick.

Rick amekutwa amejinyonga nyumbani kwake juzi, lakini hakuna taarifa sahihi zinazoeleza sababu ya msanii huyo kujinyonga.

Mtandao maarufu Sunday World, ulikuwa wa kwanza kuripoti taarifa ya msiba huo, ukieleza marehemu alikutwa amejinyonga nyumbani kwake Kaskazini mwa Johanesburg.

Vyanzo kadhaa vilivyozungumza na mtandao wa Sunday World vilidai kuwa mwanamuziki huyo, alijinyonga kwa kamba baada ya kusumbuliwa na msongo wa mawazo.





## Mliona unga mtamu, sasa mtakiona

IMEELEZWA kuwa wasanii wawili wa muziki nchini Nigeria, Zinoleesky na Mohbad, wamekamatwa na kikosi maalum cha kupambana na dawa za kulevya.

Video za wanamuziki hao zimesambaa katika mitandao ya kijamii wakionekana wapo chini ya ulinzi wa askari hao.


Kulingana na taarifa kutoka idara hiyo, katika kuwakabili wasanii hao, Zinolessky alimsukuma mmoja wa askari hao pale walipovamiwa ndani ya nyumba moja.

## Jennifer hongera kuwa mama

MWIGIZAJI wa Marekani, Jennifer Lawrence, amepata mtoto wake wa kwanza na mume wake Cooke Maroney.

Kulingana na mtandao wa TMZ, wawili hao walimpokea mtoto wao wakiwa katika jiji la Los Angeles.

Mrembo huyo ambaye ana miaka 31, akiwa ametofautiana na mume wake wa miaka sita, walifunga ndoa ya kifahari miaka miwili iliyopita katika kisiwa cha maraha cha Rhode kilichopo bahari ya Pasifiki.



MAKALA

# UKRAINE ILIPOVAMIWA KININJA

Na Mwandishi Wetu

## ■Urusi yaonyesha ubabe, yaonya atakaeingilia
## ■Marekani, Ulaya zaiacha Ukraine ikinyukwa

KWA Siku mbili mfululizo miji mbalimbali ya Ukraine, imekuwa sawa na tanuri la moto baada ya wanajeshi wa Urusi, kushambulia kila upande kwa kutumia anga, ardhini na majini.

Haijajulikana rasmi athari iliyotokea katika mashambulizi makali yanayoendelea, lakini ni wazi watu wengi watakufa, majengo yatabomolewa na miundombinu mbalimbali inateketezwa kwa mabomu.

Vita hiyo kati ya Urusi na Ukraine imekuja baada ya miezi kadhaa ya vita vya maneno kati ya nchi za Magharibi ikiongozwa na Marekani na Urusi, huku Rais Vladimir Putin, akikanusha kwamba angevamia jirani yake.

Hata hivyo, asubuhi ya Alhamisi hali ilibadilika ghafla baada ya uvamizi kuanza kwa mashambulizi makali ya mabomu kutoka katika ndege za vita na manowari za kijeshi zilizotia nanga baharini.

Kutokana na uvamizi huo, sasa Putin anashutumiwa kwa kuvunja amani ndani ya bara la Ulaya, na endapo vita hiyo ikizidi kushika kasi ni wazi usalama wa bara hilo utakuwa mashakani.

Majeshi ya Urusi wameshambulia kutoka wapi?

Katika mashambuzili ya siku ya pili, viwanja vya ndege na makao makuu ya jeshi vilipigwa mabomu. Karibu miji yote nchini Ukraine inashambuliwa pia uwanja mkuu wa ndege wa kimataifa wa Boryspil katika mji mkuu wa nchi hiyo Kyiv, nao unazidi kuharibiwa kwa mabomu.

Wakati mashambuliz ya anga yanashika kasi, vifaru na wanajeshi wa ardhini wamengia Ukraine kaskazini-mashariki, karibu na Kharkiv, jiji lenye watu milioni 1.4, ambao uko mashariki karibu na Luhansk kutoka nchi jirani ya Belarusi.

Wanajeshi walikamata kambi muhimu ya anga nje kidogo ya Kyiv, na wanajeshi wa Urusi walitua katika miji mikubwa ya bandari ya Odesa na Mariupol.

Kabla ya kuanza uvamizi huo, Rais Putin alitangazia dunia kupitia runinga kwamba Urusi haiwezi kujisikia salama, kuendelea na kuwepo kwa sababu ya kile alichokiita tishio la mara kwa mara kutoka kwa Ukraine ya kisasa.

Hoja zake zililenga kuwalinda watu wanaodhulumiwa na mauaji ya halaiki na pia kuondoa utawala wa kinazi ndani ya Ukraine. Hata hivyo Rais wa Ukraine, Volodymr Zelensky, anakana kwamba hana siasa za Nazi, pia anafananisha mashambulizi yanayofanyika ni sawa na uvamizi wa Ujerumani ya Nazi katika Vita vya Pili vya Dunia.

Rais Putin mara kwa mara amekuwa akiishutumu Ukraine kwa kuchukuliwa na watu wenye itikadi kali, tangu kiongozi wake anayeiunga mkono Urusi, Viktor Yanukovych, kuondolewa madarakani mwaka 2014.

Urusi kwa muda mrefu imekuwa ikipinga hatua ya Ukraine kutaka kujiunga na Umoja wa Ulaya na muungano wa kijeshi wa kujihami wa nchi za Magharibi Nato. Inaishutumu Nato kwa kutishia mustakabali wa taifa hilo kiusalama.



Baadhi ya raia wa Ukraine wakipata hifadhi katika kituo cha treni cha chini ya ardhi wakihofia usalama wao.

### NGUVU ZA KIJESHI

Inakadiriwa idadi ya wanajeshi wa Urusi walioingia ndani na wanaokaribia Ukraine inaweza kuwa kati ya 100,000 na 190,000.

Ijumaa iliyopita, Marekani ilisema Urusi imetuma wanajeshi kati ya 169,000 na 190,000.

Michael Carpenter, balozi wa Marekani katika Shirika la Usalama na Ushirikiano la Ulaya (OSCE), anasema idadi hiyo inajumuisha wanajeshi walioko karibu na mpaka na Ukraine, Belarus, na Crimea ambayo ilichukuliwa miaka ya nyuma.

Waziri wa Ulinzi wa Uingereza Ben Wallace, anasema asilimia 60 ya wanajeshi wa Urusi wanatoka Belarusi.

Kwa upande mwingine, Waziri wa Ulinzi wa Ukraine, ametoa idadi ya wanajeshi 149,000.

Hata hivyo, Urusi haijasema chochote kuhusu idadi ya wanajeshi wake.

Lakini Jumuiya ya kujihami ya NATO ilisema kwamba haijaona ushahidi wowote wa hii ardhini.

Wanasema kuwa theluthi mbili ya jeshi liko ndani ya kilomita 50 kutoka mpakani.

Picha za satelaiti pia zinaonyesha kuwa baadhi ya wanajeshi wa Urusi wamegawanywa katika vikundi vidogo ambao wameingia Ukraine kwa urahisi.

Uwezo wa kijeshi wa Ukraine

Jeshi la Ukraine ni dogo zaidi kuliko lile la Urusi, lakini linapata usaidizi kutoka kwa Jumuiya ya Kujihami ya Nchi za Magharibi NATO.

Marekani haijatuma wanajeshi humo, lakini imetuma wanajeshi 3,000 zaidi nchini Poland na Romania ili kuimarisha vikosi vya NATO, na imewaweka wanajeshi wengine 8,500 katika hali ya tahadhari.

Marekani pia imetuma silaha zenye thamani ya dola milioni 200, ikiwa ni pamoja na kombora la kushambulia vifaru la Javelin na kombora la kudungua ndege la Stinger. Pia imeruhusu nchi wanachama wa NATO kukabidhi silaha zilizotengenezwa Marekani kwa Ukraine.

Uingereza imepeleka makombora 2,000 ya kushambulia vifaru ya masafa mafupi nchini Ukraine, imetuma wanajeshi 350 zaidi nchini Poland, na kuongeza mara mbili uwezo wake wa kijeshi kwa kutuma wanajeshi 900 zaidi nchini Estonia.

Uingereza imetuma ndege zaidi za kivita kusini mwa Ulaya na meli ya wanamaji pamoja na wanajeshi wengine wa NATO kupiga doria bahari ya Mediterania.

Pia imewatahadharisha wanajeshi wake 1,000 ili iwapo kutatokea shambulio, wasaidie wakati wa mzozo wa kibinadamu nchini Ukraine.

Denmark, Uhispania, Ufaransa na Uholanzi pia zimetuma wanajeshi na meli zao Ulaya Mashariki na mashariki mwa Mediterania.

### URUSI ITAKWENDA MBALI NA LENGO?

Urusi imekataa kusema kama inataka kupindua serikali iliyochaguliwa kidemokrasia ya Ukraine, ingawa inaamini kwamba nchi hiyo inapaswa kusafishwa kutoka kwa Wanazi. Rais Putin alizungumzia kuwafikisha mahakamani wale waliofanya uhalifu mwingi wa umwagaji damu dhidi ya raia.

Kwa kutambua maeneo yanayoungwa mkono na Urusi yaliyojitenga ya Luhansk na Donetsk kama huru, alikuwa tayari ameamua kuwa hayakuwa tena sehemu ya Ukraine.

Jamhuri za watu wanaojiita huru zinachukua zaidi ya theluthi moja ya maeneo yote ya Luhansk na Donetsk lakini waasi wanatamani mengine pia.

### UVAMIZI UNAHATARISHA VIPI ULAYA?

Vita hiyo ni jambo la kutisha kwa watu wa bara zima la Ulaya, ikivamia nchi jirani ya Ulaya kwa mara ya kwanza tangu Vita vya Pili vya Dunia.

Makumi ya watu wamekufa tayari katika kile Ujerumani imekiita Vita vya Putin.

Viongozi wa Ulaya wamelaani kuletwa saa za giza zaidi tangu miaka ya 1940.

Emmanuel Macron wa Ufaransa, anasema uvamizi huo unaonyesha kunatakiwa hatua ya mabadiliko katika historia ya Ulaya.

Ofisa mkuu wa jeshi la Marekani, Mark Milley anasema ukubwa wa vikosi vya Urusi unamaanisha hali ya kutisha katika maeneo yenye miji mikubwa.


Uvamizi huo una madhara makubwa kwa nchi nyingine nyingi zinazopakana na Urusi na Ukraine, kama Latvia, Poland na Moldova.

Hali ya hatari imetangazwa nchini Lithuania na Moldova, ambako maelfu ya wanawake na watoto tayari wameingia kama wakimbizi.

### NCHI ZA ULAYA ZAIACHA UKRAINE

Nchi za Ulaya zimeonekana kujitenga katika vita hiyo na kubakia kuiwekea vikwazo Urusi na kuiacha serikali ya Ukraine ikipigana peke yake.

Hata hivyo, Nato imeweka ndege za kivita katika hali ya tahadhari, lakini muungano huo umeweka wazi hakuna mipango ya kutuma wanajeshi wa kivita ndani ya Ukraine. Badala yake wametoa washauri, silaha na hospitali za kutumiwa vitani.



Jengo lililoshambuliwa na bomu kutoka ndege ya Urusi likiwaka moto katika mji wa Kyiev.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAPOELEKEA

# Makosa ya watoto zamani, yaliyofanya wale bakora




**Na Adam Fungamwangwo**

SIKU hizi huwezi kukuta watoto wakipigwa bakora, si na wazazi wao nyumbani tu, bali hata mashuleni. Kuna sheria zinazolinda watoto kuchapwa tofauti na zamani ambapo, bakora ilikuwa ni kama sehemu ya maisha yao.Pamoja na kuwa na sheria za kulinda haki ya mtoto, lakini hata wazazi wenyewe siku hizi hawapo kama wale wa zamani.

Haijulikani hasa sababu ilikuwa ni nini wazazi wa zamani walikuwa na malezi ya 'kihafidhina' kwa watoto wao, lakini inawezekana ikawa ni matokeo ya athari za ukoloni zilizoachwa na Wajerumani na Waingereza walioitawala Tanganyika, ambayo kwa sasa ni Tanzania.

Inawezekana babu na baba zetu kutokana na athari za kupelekeshwa na wakoloni, wakazihamishia kwa vizazi vyao, kwani haikuwa kawaida kwa mtoto kukaa wiki bila kulamba bakora kwa makosa mbalimbali, ingawa mengine yalikuwa ya kawaida ambayo ni lazima yafanywe na mtoto.

Ndiyo maana baba au mama mkali zaidi ya kawaida wakati huo aliitwa 'Mjerumani'.

Wazazi wa sasa hadi akimpiga mtoto wake, basi kosa hilo huenda ni kubwa mno na limemgusa yeye binafsi na si vinginevyo.

Awe baba au mama, wa sasa huwezi kukuta akimuadhibu mtoto wake kwa sababu tu labda eti hajamsalimia mtu fulani "Yaani huyu mtoto ni jeuri kweli, sijui karithi tabia ya nani." Yanakuwa ni maneno ya wazazi wa sasa.

Katika hili kuna dhana mbili. Wapo wanaosema malezi ya zamani ndiyo yalikuwa malezi mazuri kwa sababu watoto walikuwa na nidhamu siyo kwa wazazi wao tu, bali kwa jamii nzima.

Hata kuporomoka kwa maadili na hata uzalendo hivi sasa, baadhi wanasema chanzo chake ni aina ya malezi ya sasa, ambapo wazazi wamekuwa wakiwalea kwa kuwadekeza watoto kupita kiasi, wenyewe wanaita 'kuwalea kama mayai'.

Wanasema hivi sasa mtoto anaweza kukuta hata wageni na wazazi wao wamekaa kwenye televisheni, akachukua 'rimoti' na kubadilisha 'chaneli', wakati zamani hata redio tu ya baba mtoto kukutwa umeishika lilikuwa ni kosa kubwa.

Inasemekana pia kuwa hivi sasa wazazi pia wamekuwa hawana muda wa kukaa na watoto zao kutokana na changamoto za maisha na kulelewa na madada wa kazi, hivyo wazazi kuwapenda kuliko kawaida watoto wao kwa muda mfupi wanaokuwa nao, wakati mwingine wasijue hata tabia zao halisi.

Wazazi wa zamani wanaelezwa kuwa walikuwa na muda mrefu wa kukaa na familia zao, kwa hiyo walikuwa wanamjua kila mmoja na tabia yake, hivyo kujipanga kukabiliana nazo kwa lengo la kumfundisha.

Upande wa pili ni wale wanaopinga malezi ya zamani. Wanadai watoto walikuwa wanaishi kama vile wako kwenye kambi za jeshi na si kwa wazazi wao.

Vipigo vilisababisha watoto hao wasijiamini na kufanya ubunifu kutokana na vipaji vyao, kwani kila wanachofanya inaonekana kama vile watakuja kupigwa.

Halafu pia wanasema vipigo vinamtia mtoto usugu kiasi kwamba anakuwa tena haogopi kupigwa, anafanya kosa akijua adhabu kubwa atakayopata ni kupigwa, ikiisha basi.

Baada ya maelezo ya pande zote mbili, tuangalie baadhi ya makosa ambayo yalikuwa yakifanywa na watoto wa miaka ya nyuma, yaliyosababisha wapigwe viboko majumbani.

Kwa wale watoto wa sasa, au vijana wanaweza kushangaa. Baadhi ya makosa ni kweli yalihitaji adhabu kama hiyo, lakini mengine kwa kizazi cha sasa kikisoma hapa kinaweza kushangaa na kucheka kwa sababu hayakuwa ya kupigwa.

Kwanza kabisa usiposalimia wakubwa asubuhi ni kosa kubwa ambalo adhabu yake ni viboko, lingine ni kutosalimia wageni, ukinawa kabla ya wageni hawajanawa wakati wa chakula.

Ukilia bila sababu unapigwa, na hata ukinyanyuka wakati au kabla wakubwa unapigwa pia, na kosa lingine ni wakubwa wakiwa wamekaa wewe, ukaenda kusimama pembeni yao.

Ukikaa wakati wakubwa wamesimama nalo ni kosa la kupigwa, ukitumwa dukani na kuchelewa kurudi ni tatizo pia.

Ukichelewa au ukiwahi kurudi shuleni yote hayo ni makosa ambayo unaweza kuishia kupigwa, ukijipitisha wakati wageni wanakula chakula, wakiondoka utapigwa pia.

Kujibujibu wakubwa hivyo ni kosa, ukiwa mbishi tatizo, ukipigwa na kulia, unalazimishwa unyamaze, la sivyo unapigwa tena, na ukipigwa umenyamaza unaonekana mjeuri, unaendelea kuchapwa ili ulie.

Wakati akinamama wa sasa wakitinga na vibwebwe shuleni kugombana na mwalimu aliyemchapa mwanaye, zamani mtoto akipigwa shuleni haendi kusema nyumbani kwa sababu anajua atapigwa tena.

Kosa lingine ni kuanza kula nyama kabla ya wakubwa, lakini pia ikibainika kuwa umekula kwa jirani bila ruhusa au kibali maalum kutoka kwenu.

Mtu mzima akipita usipomsalimia, msiposimamisha mpira wakati mkubwa anapita, akienda kusema majumbani kwenu ni balaa. Na mtu mzima akija kukuchongea nyumbani hata kama jambo si la kweli, asilimia kubwa utapigwa, kupewa pesa na mtu asiyejulikana au kuomba pesa kwa mtu yoyote yule ni fimbo.

**Tuma meseji 0716 35 05 34**

# WFP yalalamikia rushwa ya ngono

**Cabo Delgado,** MSUMBIJI

WAPOKEAJI chakula cha msaada kaskazini mwa Msumbiji, wamewalalamikia baadhi ya viongozi wa kijamii wanaohusika na usambazaji misaada hiyo, wanagawa kwa rushwa ya ngono.

Mkuu wa Mpango wa Chakula Duniani katika jimbo la Cabo Delgado, Mauricio Bortee, alifanya mkutano na viongozi wa eneo hilo siku ya Alhamisi kujadili suala hilo.

Cabo Delgado imekuwa ngome ya waasi wa jihadi tangu 2017 ambao wamewafanya maelfu ya watu kutoroka makwao.

"Malalamiko tuliyopokea yanahusu viongozi wa kijamii wanaotumia vibaya au kubadilishana chakula kwa ngono," alisema.

Alisema WFP haiwezi kuvumilia ukiukwaji kama huo, Bortee alieleza lengo la shirika hilo ni kutoa misaada kila wakati bila kuwadhuru watu wanaowahudumia na ndio maana wako huko kushughulikia maswala hayo, kwa kushirikiana na washikadau wengine.

## Msichana ahukumiwa kifungo kusababisha vifo

**NAIROBI.** KENYA

MSICHANA mmoja raia wa Kenya, amehukumiwa kifungo cha miaka mitano jela kwa kosa la kuua bila kukusudia kufuatia tukio la moto lililochoma bweni la shule na kuua wanafunzi tisa.

Mshtakiwa huyo ambaye naye ni wanafunzi wa shule hiyo (18), alifanya kosa hilo mwaka wa 2017 akiwa na umri wa miaka 14 katika mwaka wake wa kwanza wa shule ya upili katika Shule ya Wasichana ya Moi iliyopo mji mkuu wa Nairobi.

Mahakama ilikuwa imefahamishwa kwamba alijaribu kujiua mara mbili kabla ya kuwasha moto ndani ya chumba chake cha kulala.

Wazazi na walezi wa wasichana waliofariki katika tukio hilo walisema hukumu hiyo ni ndogo lakini wanafurahi kwamba haki imetendeka.

Visa vya uchomaji moto vimekuwa tatizo la kawaida katika shule za bweni nchini Kenya katika miongo miwili iliyopita.

**HABARI ZOTE BBC**



Vikosi vya Urusi vikiingia ndani ya mitaa ya mji wa Kyiv nchini Ukraine baada ya mapambano makali. **PICHA: USA TODAY**

# Urusi yazidi kuiangamiza Ukraine, raia walala vituo vya treni kujinusuru

**KYIV,** UKRAINE

MASHAMBULIZI makali kutoka majeshi ya Urusi yamechukua siku ya tatu, huku serikali ya Ukraine ikidai maeneo ya raia yanalengwa na vikosi hivyo.

Ofisa wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi hiyo, Vadym Denysenko, alisema si kweli Warusi hawalengi sehemu zilizo na raia, lakini kuna maeneo 33 ya raia yameshambuliwa katika kipindi cha saa 24 zilizopita.

Vikosi vya Urusi vimeufunga mji mkuu Kyiv, baada ya kusonga mbele kwa kasi kutoka pande tofauti za kaskazini, mashariki na kusini mwa Ukraine tangu uvamizi huo uanze siku ya Alhamisi.

Maofisa wa Ukraine walisema wanajeshi wa Urusi tayari wako katika jiji hilo, wakiwataka wenyeji kupigana na mabomu ya petroli.

Huku hayo yakijiri, Rais wa Ukraine, amepongeza juhudi zinazofanywa na wale wanaoitetea nchi yao.Alipongeza ushujaa wa askari na raia ambao wanapambana dhidi ya wavamizi. Takriban raia 137 wa Ukraine waliuawa siku ya kwanza ya vita.

Ukraine imetoa wito kwa raia wote wanaoweza kubeba silaha kuungana katika ulinzi wa nchi yao.

### RAIA WAKIMBILIA VITUO VYA TRENI

Wakazi wengi katika miji mbalimbali ya Ukraine wamekimbilia vituo vya treni vya chini ya ardhi kuepuka mashambulio kutoka vikosi vya Urusi.

Picha zinaonesha mamia ya wananchi hao wakiwemo watoto na wazee, wakilala katika vituo vya treni katika miji ya Kyiv na Kharkiv.

Wengi wao wamejifunika blanketi na kuvalia nguo za kuzuia baridi wakiwa wamezungukwa na mabegi yaliyohifadhi vitu vyao binafsi.

Amri ya kutotoka nje usiku iliwekwa nchini humo, na vituo vya treni viliendelea kuwa wazi ili kutumika kama vihifadhi vya mabomu.

### RAIS AISHTUMU ULAYA KUWATELEKEZA

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, aliwashutumu viongozi wa Ulaya kwa kutochukua hatua za kutosha kupunguza kasi ya Urusi kuvamia nchi yake.

Akizungumza kutoka ofisini kwake mjini Kyiv, akiwa amevalia sare za kijeshi alisema magari ya kivita na mashambulio ya angani ni sawa na kile Ulaya ilishuhudia wakati wa Vita Vikuu vya Pili vya Dunia.

Alisema ni kinyume na walichosema hakitawahi kutokea lakini kinatokea, hata hivyo aliongeza kuwa bado hawajachelewa kukomesha uchokozi wa Urusi ikiwa viongozi wa Ulaya watachukua hatua haraka.

Wakati huo huo, kiongozi huyo ametoa ombi jingine kwa washirika wa nchi za Magharibi kuisaidia Ukraine na kukomesha mashambulizi ya kikatili ya Urusi.

"Leo asubuhi tunalinda taifa letu peke yetu. Kama jana, majeshi yenye nguvu zaidi duniani yanatazama kutoka mbali," Zelensky alisema katika hotuba yake kwa taifa asubuhi ya jana.

Aliongeza "Je, Urusi ilishawishika na vikwazo vya jana? Tunasikia katika anga yetu na kuona kwenye ardhi yetu kwamba hii haitoshi."

Kiongozi wa Ukraine amethibitisha mashambulio mengi ya makombora yaliyoripotiwa alfajiri ya jana. Zelensky alisema mashambulizi hayo yalianza saa kumi asubuhi kwa saa za huko. Aliongeza kuwa mashambulizi ya Urusi yalilenga maeneo ya kijeshi na ya kiraia.

Urusi hapo awali ilisema hailengi maeneo ya raia.

Mji mkuu wa Kyiv umeshuhudia milipuko mingi ya mabomu, ikiwa ni pamoja na kile kinachoonekana kuwa shambulizi lililolenga jengo la makazi ya raia.

### CHINA YAIUNGA MKONO URUSI

Wakati nchi za Magharibi zikiungana kuipinga Urusi, lakini jirani yake China haijachukua msimamo mkali.

Kupitia njia ya simu, Rais Xi Jinping alimwambia mwenzake wa Urusi Vladimir Putin, kwamba China inamuunga mkono katika juhudi za kutatua mgogoro wa Ukraine kupitia mazungumzo, televisheni ya taifa ya China CCTV inaripoti.

Mzozo wa Ukraine na Urusi unaleta changamoto kubwa kwa China katika nyanja tofauti.

Uhusiano wa karibu zaidi wa kidiplomasia kati ya Urusi na China unaweza kuonekana kwenye michezo ya majira ya baridi wakati Putin alipozuru nchi hiyo kama mmoja wa viongozi wachache duniani waliohudhuria.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## TANGAZO KUPOTEA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

**Kapingu Magina** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba 406 kitalu "jj" kilichopo Ndembezi Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Kapingu Magina kwa simu namba **0786-499533**

**Rbnamba Shy/RB/3754/ 2018.**

MUSA J. MAKUNGU
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA
AFISA ARDHI WA MANISPAA SHINYANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GLADYS GEORGE YAMBESI** anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari aina ya **LAND CRUISER PRADO** yenye USAJILI NAMBA **T562 CCQ,** CHASIS NAMBA **R2J1200024439,** ENGINE NAMBA **2R26179787.** Kwa yeyote atakeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: -
**DAR/MAG/RB/80114/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BENJAMIN PASCHAL KILANGWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato che nne chenye index namba **S.4486-0025** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MALIMBE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/80678/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PAULINE ALEXANDER** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV 4** yenye USAJILI NAMBA **T631 CEF,** CHASIS NAMBA **JTEHH20V500218000,** ENGINE NAMBA **1AZ1019824.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: -
**KU/RB/6I81/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BARAKA AMIRI MARADONA** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T671BDE , Engine **No.3S9318564** Chassis No. **SXA110117479** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Taarifa ya polisi
**KIL/MWA/RB/78223/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LISA GODFREY KISHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST** yenye namba za usajili **T 347 DQJ,** chasis namba **NCP1100022745,** engine namba **IN2D561298,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DOD/DOD/RB/81460/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**NDUGU SHAHIBU RAMADHAN QUDRA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Trekta yenye namba za usajili **T674DCT** aina ya **MASEY FERGUSON** Rangi Nyekundu yenye Chasis No. **1652160590.**Engine **No.5238874**
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba **DOD/DOD/RB/81410/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LUSEKELO JAMES MWAKALUKWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **LANDROVER DISCOVER** yenye namba za usajili **T 806 BMN** , chasisi namba SALLT**AM231A730180,** engine namba **56D53022A,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**ARU/ARU/RB/80496/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba, Kituo cha Mahakama ya Mwanzo Bukoba Mkoa wa Kagera.**

**Shauri la Madai Na. 24/ 2021**

**Jina la Mdai ............................JORO MICROFINANCE**

**Jina la Mdaiwa........................SAID A. MASANYIWA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**

Kwa SAID A. MASANYIWA, Kwamba Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 14 Mwezi 03 Mwaka 2022, kueleza kwa nini hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 14 Mwezi 02 Mwaka 2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA.**

**MAOMBI MADOGO NA. 281/2021**

**PASCHAL GABRIEL ............................................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**ELIAS KAIZILEGE .........................................MJIBU MAOMBI**

**KWA: ELIAS KAIZILEGE (POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa Maombi Madogo Na. 281/2021 yamepangwa kutajwa tarehe 23/03/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 19/01/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NO.301/2019**

**ISACK KABUJE::::::::::::::::::::::::MDAI**

**DHIDI YA**

1. **GOODLUCK CHELESTINO KIGWILE:::::MDAIWA**
2. **GAMBO JOHN MILINGA::::::::::::::::::::::::MDAIWA**
3. **CONFORT MWAKIJILA::::::::::::::::::::::::MDAIWA**

**YAH:KUITWA SHAURINI**

**KWA: GAMBO JOHN MILINGA,**

Fahamu kwamba **ISACK KABUJE** amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 03/03/2022,saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.
Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 15/02/2022.

Y. Munzerere
MWENYEKITI
15/02/2022.

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake.
Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni namba moja-15




**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

Kilichobakia mfukoni ni bastola. Ile aliyoiazima kutoka kwa mjomba Ken.

Sekunde chache baadaye makali ya kisu yalipenya kwenye mwili wa jamaa. Aliguna, lakini si kwa sauti.

Jan alichomoa na kukita tena ndani ya mwili. Safari hii nguvu zilimwishia mtu yule. Akatii kila alichofanya Jan. Alimlaza chini taratibu na kummalizia kwa pigo la tatu.

Ingawa hakutaka mwezake asikie, lakini kishindo kidogo kilisikika, ambacho kilimfanya mtu wa pili kugeuka nyuma. Hakuona kitu.

Tayari mwili wa mwenzake ulikuwa umelala chini kwenye majani, huku Jan pia akilala kifudifudi.

"Nilikwambia Sele, usipite huko, angalia unavyojikwaakwaa, utanikuta mbele." Sauti ya mwenzake ilisikika.

Jan alitulia tuli. Alijua kuwa sasa amebaki mmoja. Hata hivyo hakujidanganya kama ni kweli amebaki yeye tu. Alichodhani ni kwamba ni lazima kutakuwa na watu wengine. Ama wanafuatilia mwenendo wote, au wanasubiri mzigo na hasa juu ya daraja.

Hata hivyo alijipongeza kwa wazo wale hilo, kwani wazo la pili ilikuwa ni kumuacha kupambana nao, baada ya kuchukua mkoba wa pesa. Aliliona halina maana, ndiyo maana akaamua kummaliza.

Akili yake ilianza kufanya kazi haraka sana kwani tayari kama ni kazi, alikuwa ameshaingia kazini.

Kummaliza wa pili ilikuwa nia yake. "Kama atachukua mkoba na kurudia huku itakuwa ni kazi rahisi sana. Lakini akitokea upande wa pili utakuwa ni mtihani." Alijiambia huku akimshuhudia mtu aliyebaki akiwa amefika kwenye mkoba, ambao uliwekwa chini ya nguzo ya katikati ya daraja hilo la Kajima.

Wakati akiinua mfuko tu. Kuna sauti ilisikika kutoka upande ambao Jan hakujua ni upi.

"Weka huo mkoba chini na unyooshe mikono juu." Ilikuwa ni sauti nzito yenye amri.

Ni sauti iliyomugopesha jamaa, akasalimu amri, kwani hakujua aliyezungumza hivyo yuko wapi na ana silaha gani.

Kwa macho yake, alishuhudia mtu mmoja, mnene mfupi akiwa na bastola. Alijitokeza na kusimama hatua kadhaa kutoka alipokuwa yule mtu wa kwanza.

Hapo hapo akajitokeza mtu wa tatu. Yeye ndiye aliyekwenda kuuchukua mkoba huo. Alipofanya hivyo akarejea karibu na mwenzake. Kitendo bila kuchelewa, jamaa mfupi mnene alifyatua bastola iliyompeleka chini jamaa kama gunia la mtama.

**"Weka huo mkoba chini na unyooshe mikono juu." Ilikuwa ni sauti nzito yenye amri.**

Mlio wa risasi hiyo ulionekana kuharibu hali ya utulivu na upweke uliokuwa eneo hilo, huku juu gari moja moja tu ilionekana kupita.

Haya yote yalitokea mbele ya macho ya Jan. Yalikuwa ni mambo ya kutisha ambayo hakupata kukutana nayo kwenye maisha yake. Aliona kana kwamba anaangalia sinema moja ya kutisha. Lakini huo ndiyo ukweli wenyewe. Yeye mwenyewe tayari alikuwa ameshaua mtu mmoja.

"Simameni hapo hapo. Mikono juu." Ilikuwa ni sauti nyingine tena.

Jan, alishindwa kuelewa ni nini kimetokea? Ni kwa nini kumekuwa na watu au makundi yaliyojua juu ya jambo hilo tofauti na ilivyokuwa awali kwenye daraja la Mfugale.

Waliojitokeza sasa walikuwa ni askari. Mmoja aliwaamuru wale vijana wawili mmoja adondoshe mkoba na mwingine bastola. Wakafanya hivyo. Askari polisi wawili walionekana kuwafuata kwenda kuwasachi, huku mmoja akiwalinda.

Katika namna ya ajabu, yule jamaa mnene mfupi aliruka juu, kama mcheza sarakasi kubingirika hatua kadhaa mbele, hapo hapo risasi kadhaa zikimkosa, akatokemea kwenye kichaka ambacho Jan alikuwa amejificha.

Hakukuwa na utulivu tena, risasi zilipigwa, zingine bila mpangilio maalum. Jan hakujitikisa kwenda mbele wala nyuma. Alipokuwa amejificha alipaona ni sehemu salama zaidi kuliko popote pale atakapokwenda. Na wala hakujidanganya kutoka, kwani asingeaminika kwa kundi lolote, liwe la majambazi watekaji, au maaskari.

Kitu pekee alichokuwa na uhakika nacho ni kwamba wale askari aliowaambia waje ndiyo wamefika, lakini wamekutana na watekaji.

Wakati huo, tayari watu kadhaa walikuwa wamelala chini, wakiwemo askari wawili. Watekaji wengine nao walijitokeza. Ina maana kulikuwa na askari na watekaji wengi tofauti na alivyodhani.

Ilionekana kundi la watekaji lilikuwa limezidiwa na askari polisi wanne walikuwa chini maiti na wengine wawili majeruhi, huku wao wakipoteza maafande wawili.

"Juu huko, tunaomba nguvu ya maaskari wawili." Afande mmoja alisikika akiongea na simu ya upepo.

Ghafla walitokea maaskari wawili. Walipita eneo ambalo alikuwa karibu na jamaa yule mfupi mnene ambaye alikuwa amejificha, huku askari wakidhani amekimbia.

Pamoja na kwamba kulikuwa na giza, lakini Jan aliuona mkono wa jamaa yule ukiinuka ukiwa na bastola.

Bila ya kuwaza na yeye alitoa bastola. Milio miwili ya bastola iliyoonekana imeachana sekunde iliwashangaza askari polisi. Ni kwa sababu haikutoka kwao na tayari walikuwa wameshawadhibiti wahalifu wote. Wakati wakitafakari la kufanya, mlio mwingine wa risasi ukasikika. Sasa ilibidi wote walale chini kwani waliona wamevamiwa na kundi lingine la wahalifu.

Ukweli ni kwamba ni kazi iliyofanywa na Jan. Wakati akimlenga askari mmoja, papo hapo na yeye akaamua kumpiga, ili asimuue askari, lakini alikuwa amechelewa sekunde moja, kwani tayari alikuwa amefyatua risasi. Hata hivyo ilimkosa askari aliyekusudiwa na Jan mwenyewe hakumlenga ipasavyo yule jamaa aliyejificha.

Ilionekana baada ya kujeruhiwa, jamaa yule aligeuka na kutaka kujua ni wapi risasi hiyo ilipigwa kutoka nyuma yake. Ndipo alipompa sura vizuri Jan, akamtandika kwenye paji la uso.

Kwa kazi aliyoifanya, aliona sasa hakuwa na sababu ya kuendelea kujificha. Alikuwa na uhakika kuwa askari watamtambua kuwa yeye ndiye aliyewataarifu na pia ndiye alikwenda kuweka mkoba ule pale. Kosa lake moja tu ni kwamba hakuondoka sehemu hiyo ya hatari. Kitendo cha kuwasaidia na kuwaponya kuuawa, pia kungemfanya kuonekana shujaa mbele ya askari polisi.

Alitafuta njia ya kutaka kujitokeza akashindwa. Vyovyote vile ambavyo angejitokeza, angeonekana ni mmoja wao, hivyo angepata zawadi ya risasi.

Alifikiri kidogo, akapata wazo. Akaweka bastola yale mfukoni na kupachika kisu chake kiunoni. Akasimama na kutembea taratibu hadi sehemu ambayo hakukuwa na kichaka cha majani yaliyokuwa pembezoni mwa kingo za daraja la Kajima.

Akanyanyua mikono juu na kujitokeza mbele ya askari waliokuwa wamelala chini, kila mmoja akitafakari jinsi walivyovamiwa na watu wengine.

"Ni mimi afande. Ni mimi niliyeweka mkoba wa pesa hapo kwenye daraja na mimi ndiye niliyewaita." Alijitokeza huku akiwa ameweka mikono juu.

"Nilikuwa nimejificha kwenye kichaka hiki, huku nimeua majambazi wawili, mmoja ni yule jamaa mfupi aliyewakimbia hapo, alikuwa amejificha pale na yeye alikuwa anataka kuwaua, nimempiga bastola."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# DOKII ASAKA SH. MILIONI 55 KUANDAA SAMIA MARATHON

**Na Sabato Kasika**

MSANII aliyewahi kutamba katika maigizo na vichekesho hapa nchini, Ummy Wenceslaus 'Dokii' amesema anahitaji kupata Sh. milioni 55 kutoka kwa wadau mbalimbali ili kuandaa mbio maalum zitakazojulikana kwa jina la 'Samia Marathon'.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Dokii alisema lengo la kuanzisha mbio hizo ni kuionyesha jamii hata mwanamke ana uwezo wa kuongoza nafasi ya urais katika taifa lolote.

Dokii alisema anaamini pia kupitia mbio hizo, wanariadha chipukizi hasa wanawake watajitokeza kwa wingi kwa sababu ya kuvutiwa na jina la shindano hilo.

"Ni wazo ambalo nimelianzisha, ninatafuta wafadhili wa kunipata kiasi hicho cha fedha ili ikiwezekana niratibu mbio hizo, basi naomba niruhusiwe kuonana na Rais Samia nimweleze nia yangu hiyo aone jinsi ya kunisaidia ili nifanikishe,"alisema Dokii.

Msanii huyo aliongeza anakusudia Samia Marathon kuwa mbio za wanawake tu endapo atafanikiwa kupata fedha, shindano hilo litaanzia Dar es Salaam na baadaye litahamia katika mikoa mingine kulingana na ratiba itakavyopangwa.

"Ninatamani hata nikifa, niache alama kwamba nilichangia jamii kutambua mchango wa mwanamke katika maendeleo ya nchi hii, kwani Rais Samia ametuheshimisha wanawake kwa kuonyesha tunaweza," Dokii alisema.

Aliongeza wakati akiendelea kusaka wafadhili, ndoto yake kubwa ni kuonana na Rais Samia ili kujadili kwa kina lengo lake hilo kama njia mojawapo ya kuendelea kutambua mchango wa mwanamke katika maendeleo ya taifa hili. Msanii huyo alisema pia matamanio yake na nguvu zake kwa sasa yapo katika kutafuta wafadhili wa kumpa fedha ili kufanikisha lengo lake la kuandaa shindano la Samia Marathon ambalo litakuwa bora hapa nchini.

"Nikipata kianzio hicho tu cha Sh. milioni 55, kinatosha kwani kadri shindano litakavyokuwa linafanyika, ninaamini wafadhili wengi zaidi watajitokeza kudhamini na kufikia malengo ya kitaifa," alisema msanii huyo.

Dokii ni miongoni mwa wasanii waliojizolea umaarufu kwa jinsi alivyoweza kuigiza katika lafudhi ya kiswahili cha nchi jirani ya Kenya, ambapo ilifikia baadhi ya watu kuamini si Mtanzania.




Rais wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Wallace Karia (aliyesimama), akizungumza katika mkutano mkuu wa baraza hilo uliofanyika jijini Arusha jana na kuhudhuriwa na marais kutoka nchi wanachama wa ukanda huo. **PICHA: TFF**

# Wasichana U-17 wajifua Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 inaendelea vyema na mazoezi yake kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia U-17 dhidi ya wenzao kutoka Botswana.

Yosso hao wa Tanzania watawakaribisha wenzao kutoka Botswana katika mechi ya kwanza itakayochezwa Machi 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Timu hizo zitarudiana kati Machi 17 na 19, mwaka huu jijini Gaborobe, Bostwana ambapo mshindi wa jumla atasonga mbele.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime, alisema wachezaji wake wanaendelea vizuri na programu ya mazoezi kama alivyopanga na anafurahi kuona viwango vya nyota wake vinazidi kuimarika.

Shime alisema timu hiyo inafanya mazoezi mara mbili kwa siku na anaamini iko katika nafasi nzuri ya kuanza vyema safari ya kuelekea kwenye fainali hizo za Dunia zitakazochezwa India hapo mwakani.

"Timu inaendelea vizuri na hali ya hewa ya Zanzibar haina tofauti sana na ile ya Tanzania Bara, mpaka sasa wachezaji wapo vizuri na wote wanafanya mazoezi kwa mujibu wa mpangilio wa mazoezi ambao kama kocha nimeupanga," alisema Shime.

## UMZ, Bungi Sisters kufungua pazia

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya UMZ inatarajia kuvaana na Bungi Sisters katika mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar msimu wa 2021/2022 itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Bungi ulioko Mkoa wa Kusini Unguja.

Bingwa wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 10 atapata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki msimu huu.

Timu zinazoshiriki ligi hiyo ni pamoja na Bungi Sisters, Dunga Queens, Warriors Queens, Green Queens, New Generation, UMZ, Yellow Queens, Future Queens zote kutoka Unguja huku Wete Sisters na Mkoani Queens zinatoka Pemba.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Wanawake Zanzibar, Ali Ussi, alisema maandalizi yote kuelekea mchezo huo wa ufunguzi yamekamilika na kuongeza ligi hiyo itachezwa katika kituo kimoja cha Unguja.

"Timu mbili za kutoka Kisiwani Pemba zitawasili Unguja kuanzia siku ya Jumamosi, hii inatokana na ligi kuchezwa katika kituo kimoja pekee," alisema Ussi.

## Ngome yapania kutetea ubingwa

**Na Saada Akida**

TIMU ya mpira wa mikono ya Ngome imesema imejipanga imara kuhakikisha inaibuka mabingwa wa mashindano ya Klabu Bingwa Taifa yatakayofanyika kuanzia Machi 23 hadi 28, mwaka huu katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa Ngome, Shazir Issa, alisema wanaendelea vizuri maandalizi ambapo watatumia wiki moja kuweka kambi kabla ya kuelekea katika michuano hiyo.

Shazir alisema anaamini timu yake itafanya vizuri katika mashindano huku akiweka wazi maandalizi hayo yatakuwa na awamu tatu ambapo wataanza na mazoezi ya gym halafu wataenda ufukweni na kumalizika na kucheza mechi za kirafiki.

"Tutakuwa na mechi sita za kirafiki, wanaume watacheza michezo mitatu na wanawake tatu, tunatarajia kwenda Zanzibar kwa ajili ya kucheza michezo hiyo," alisema Shazir.

Alisema watahakikisha ndani ya wiki moja wanamaliza programu yao hiyo yenye awamu tatu kwa ajili ya kuwa imara na hatimaye kwenda kutetea ubingwa wanaoushikilia.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LUKAKU KURUDI INTER
MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Romelu Lukaku amehusishwa na kurejea katika klabu yake ya zamani Inter Milan, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28 anataka kusalia na kupigania nafasi yake Stamford Bridge. ***(Mirror)***

### HAALAND ANUKIA CITY
MANCHESTER City wanaongoza katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland kutoka Borussia Dortmund msimu huu wa joto, wakati Barcelona, Bayern Munich, Paris St-Germain na Real Madrid pia wametoa ofa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. Real wanataka Haaland abaki Dortmund kwa msimu mmoja zaidi kabla ya kumsajili. ***(SER Deportivos)***

### HATIMA YA HAALAND YAJA
MKURUGENZI wa Michezo wa Dortmund, Hans-Joachim Watzke anatarajia mustakabali wa Erling Haaland katika klabu hiyo ya Ujerumani kuamuliwa katika muda wa wiki sita zijazo. (RTL)

### MBAPPE AIGOMEA PSG
MKATABA wa mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe na Paris St-Germain unamalizika msimu wa joto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 amekataa ofa nyingine katika klabu hiyo. (Marca)

### DYBALA NJIA MOJA
ARSENAL, Chelsea, Manchester City, Manchester United na Tottenham Hotspur zinavutiwa na mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala mwenye umri wa miaka 28, ambaye yuko tayari kuondoka Juventus wakati mkataba wake na timu hiyo ya Serie A utakapokamilika msimu wa joto. ***(90min)***

### RUDIGER AKARIBIA UNITED
KLABU ya Manchester United ina nia ya kumsajili mlinzi wa kati wa Ujerumani, Antonio Rudiger kwa uhamisho wa bure wakati mkataba wake na Chelsea utakapokamilika msimu wa joto na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 atachelewesha uamuzi hadi mwisho wa msimu. ***(Mirror)***

### UNITED YAMFUATA AKANJI
MANCHESTER United wana nia ya kumsajili mlinzi, Manuel Akanji kutoka Borussia Dortmund na inasemekana tayari wamewasilisha ofa kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi mwenye umri wa miaka 26. ***(Bild)***

### DEMBELE KUTUA CHELSEA
CHELSEA wamefutilia mbali jaribio la kumnunua winga wa Bayern Munich na Ujerumani, Serge Gnabry mwenye umri wa miaka 26 na badala yake itamsajili mshambuliaji wa Barcelona na Ufaransa, Ousmane Dembele (24). ***(Sport)***

### FLETCHER HUYO MAREKANI
MSHAMBULIAJI wa Watford, Ashley Fletcher mwenye umri wa miaka 26, anakaribia kujiunga na klabu ya Ligi Kuu ya Marekani, New York Red Bulls kwa mkataba wa mkopo. ***(Sun)***

### MARTINEZ AFURAHIA INTER
WAKALA wa mshambuliaji wa Argentina, Lautaro Martinez, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United na Barcelona, amesema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 "anafuraha" katika klabu ya Inter Milan. ***(FcInternews.it)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# DYBALA ANUKIA KUTUA ENGLAND

Ni baada ya mshambuliaji huyo kusema anataka kuondoka Juve ingawa…

**TURIN, Italia**

KLABU kadhaa za Ligi Kuu England maarufu EPL ziko katika mazungumzo na wawakilishi wa Paulo Dybala, baada ya mchezaji huyo kuweka wazi yupo tayari kuondoka Juventus mara mkataba wake utakapomalizika kipindi cha majira ya joto.

Chelsea, Arsenal, Manchester City, Manchester United na Tottenham Hotspur zote zimeanza mazungumzo ya wazi na mawakala wa mchezaji huyo na wamethibitisha kumtaka nyota huyo.

Hata hivyo, klabu hizo bado zina wasiwasi kama Dybala mwenyewe atakuwa tayari kuhamia katika Ligi Kuu England, licha ya mchezaji huyo na wasaidizi wake kusema ana nia ya kuondoka kule Turin.

Daily Mail iliripoti mwezi uliopita kwamba, licha ya nyota huyo kutaka kuondoka, lakini bado anaweza kusaini mkataba mpya na Juventus.

Raia huyo wa Argentina alikuwa katika mazungumzo na Juventus kuhusu kuongeza mkataba mpya wa miaka mitano wenye thamani ya euro milioni nane kwa mwaka kabla ya Krismasi iliyopita.

Lakini baada ya masharti hayo kubadilishwa na Juve dakika za mwisho kutokana na rekodi ya fowadi huyo kuwa na majeruhi ya mara kwa mara, mazungumzo yalivunjika.

Licha ya uwezekano wa kusaini mkataba mpya katika klabu yake ya sasa, inaelewaka Dybala pia ana chaguo la kubakia Serie A kwa kujiunga na Inter Milan.

The Nerazzurri ni miongoni mwa timu zilizoonyesha nia ya kutaka kumsajili mchezaji huyo wakati mkataba wake wa sasa utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu.

Uhamisho wowote unaowezekana kwenda Inter unaweza kufungua njia kwa raia mwenzake Lautaro Martinez kuondoka Serie A msimu huu wa joto.

Mshambuliaji huyo wa Inter amekuwa akivutiwa na Tottenham, City na Arsenal siku za nyuma - ambao 'walichunguza' uwezekano wa kumsajili Lautaro katika dirisha la usajili la majira ya joto la 2021.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 961,

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
WATFORD
1 | 1.37
X | 4.84
2 | 8.00

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# XAVI ASIFU KIWANGO CHA WACHEZAJI WAKE

**NAPLES, Italia**

XAVI anaamini Barcelona walicheza kwa "kiwango bora zaidi kwa msimu huu" wakati wa mchezo wa pili wa raundi ya mtoano ya Ligi ya Europa dhidi ya Napoli.

Blaugrana walitinga hatua ya 16 bora ya mashindano hayo baada ya kukamilisha ushindi wa jumla wa mabao 5-3 kutokana na ushindi wa magoli 4-2 kwenye Uwanja wa Stadio Diego Armando Maradona, Alhamisi.

Mabao ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Jordi Alba, Frenkie De Jong na Gerard Pique yaliwaweka wageni udhibiti mjini Naples, huku Pierre-Emerick Aubameyang akafunga la nne.

Barca walipiga mashuti 16 kwa saba ya wapinzani wao, huku wakitawala mechi kwa asilimia 56.

"Labda, hiki kilikuwa kiwango bora zaidi kwa msimu wetu," alisema Xavi akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Tulitaka kutawala na tulifanya hivyo.

"Nimefurahishwa na juhudi tulizoweka na soka tulilocheza, matokeo yake ni ya haki.

"Nina furaha sana kwa wachezaji. Tuko kwenye njia sahihi."

# Arteta: Arsenal sasa inaimarika

**LONDON, England**

MIKEL Arteta hakuwa na tatizo na Arsenal kuiacha ikichelewa kushinda Wolves siku ya Alhamisi, akipendekeza ushindi huo mkubwa ulikuwa mzuri kwa mazingira ya timu yake.

Arsenal walisherehekea ushindi muhimu wa mabao 2-1 katika harakati zao za kufuzu katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Emirates.

Washikabunduki hao walipanda hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pointi moja nyuma ya Manchester United walio nafasi ya nne wakiwa na michezo miwili mkononi.

Wakifuatia bao la kwanza la Hwang Hee-chan, vijana wa Arteta hatimaye walisawazisha kupitia Nicolas Pepe, ambaye pia alicheza vizuri na Alexandre Lacazette na kupata bao la ushindi ambalo lilikuwa la kujifungwa kwa Jose Sa.



Bao hilo la kujifunga liliingia dakika 94 na sekunde 56, na kuifanya Arsenal kuondoka na pointi zote tatu.

Alipoulizwa kama angependelea kuiona Arsenal katika ushindi wa kawaida, Arteta aliiambia Prime Video: "Labda (ningependelea) jinsi tulivyoshinda, kwa sababu inajenga imani kama hiyo, umoja, hali ya hewa na mshikamano na mashabiki wetu. vizuri.

"Hiyo ni muhimu sana. Tunataka sana kuunda kitu maalum hapa, na bila mashabiki wetu hatutaweza kufanya hivyo."

Arsenal sasa wameshinda michezo saba kati ya tisa iliyopita ya Ligi Kuu England, wakipoteza mechi moja tu.

HABARI MICHEZO

,840,460

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/02/22 | 18:00 | Brighton vs Aston Villa | 2.32 | 3.25 | 3.10 |
| 02. 26/02/22 | 18:00 | Brentford vs Newcastle | 2.41 | 3.25 | 2.95 |
| 03. 26/02/22 | 18:00 | Peterborough vs Hull City | 2.54 | 3.12 | 2.73 |
| 04. 26/02/22 | 18:00 | Millwall vs Sheffield Utd | 2.85 | 3.20 | 2.40 |
| 05. 26/02/22 | 18:00 | Birmingham vs Huddersfield | 2.50 | 3.24 | 2.70 |
| 06. 26/02/22 | 19:00 | Sivasspor vs Besiktas | 2.56 | 3.05 | 2.81 |
| 07. 26/02/22 | 20:30 | Oostende vs St Truiden | 2.47 | 3.40 | 2.66 |
| 08. 26/02/22 | 22:45 | Sassuolo vs Fiorentina | 2.75 | 3.44 | 2.47 |
| 09. 27/02/22 | 14:15 | AZ Alkmaar vs Feyenoord | 2.52 | 3.50 | 2.52 |
| 10. 27/02/22 | 15:30 | Hamburger SV vs Werder Bremen | 2.43 | 3.44 | 2.65 |
| 11. 27/02/22 | 16:00 | Alanyaspor vs Konyaspor | 2.45 | 3.16 | 2.86 |
| 12. 27/02/22 | 17:00 | Angers vs Lens | 2.80 | 3.25 | 2.50 |
| 13. 27/02/22 | 17:00 | Metz vs Nantes | 2.78 | 3.13 | 2.59 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 26/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4427 | Nizhny Novgorod vs Ural Yekaterinburg | 2.65 | 3.00 | 2.70 |
| 15:00 | 2793 | Nairobi City Stars FC vs Mathare United | 1.21 | 5.37 | 11.52 |
| 15:00 | 4312 | Ulinzi Stars vs Kenya Commercial Bank | 3.18 | 3.13 | 2.15 |
| 15:00 | 4585 | Kenya Police vs Wazito | 1.73 | 3.42 | 4.33 |
| 15:30 | 3412 | Blackburn vs QPR | 2.12 | 3.19 | 3.39 |
| 15:30 | 5496 | Leeds vs Tottenham | 3.75 | 3.85 | 1.87 |
| 15:45 | 2048 | Barry Town FC vs Caernarfon Town | 2.35 | 3.56 | 2.55 |
| 16:00 | 1683 | Prison Leopards vs Kabwe Warriors | 2.38 | 2.60 | 3.38 |
| 16:00 | 2979 | Kafue Celtic FC vs Lusaka Dynamos | 2.27 | 2.61 | 3.62 |
| 16:00 | 3351 | Mbeya Kwanza FC vs Mtibwa Sugar | 2.07 | 2.80 | 3.86 |
| 16:00 | 3980 | Mallorca vs Valencia | 2.45 | 3.15 | 3.00 |
| 16:00 | 4557 | Green Buffaloes vs Zesco United | 2.43 | 2.77 | 3.06 |
| 16:00 | 4742 | Juve Stabia vs Monopoli | 2.71 | 2.96 | 2.76 |
| 16:00 | 5312 | Standard Liege W vs Genk W | 1.66 | 4.06 | 3.96 |
| 16:30 | 2969 | Dornbirn vs FC Juniors OO | 2.36 | 3.42 | 2.60 |
| 17:00 | 3168 | Pogon Szczecin vs Lech Poznan | 2.60 | 3.03 | 2.60 |
| 17:00 | 4504 | Salernitana vs Bologna | 3.30 | 3.30 | 2.20 |
| 17:30 | 1621 | Union Berlin vs Mainz | 2.63 | 3.13 | 2.73 |
| 17:30 | 2216 | Greuther Furth vs FC Koln | 3.43 | 3.63 | 2.01 |
| 17:30 | 4189 | Monchengladbach vs VfL Wolfsburg | 2.07 | 3.44 | 3.44 |
| 17:30 | 4241 | SC Freiburg vs Hertha BSC | 1.59 | 4.09 | 5.18 |
| 18:00 | 1145 | Akwa Starlets FC vs Lobi Stars | 1.87 | 3.25 | 4.60 |
| 18:00 | 1847 | All Stars vs Hearts of Oak | 3.76 | 2.84 | 2.07 |
| 18:00 | 2638 | Manchester Utd vs Watford | 1.37 | 4.84 | 8.00 |
| 18:00 | 2788 | Brighton vs Aston Villa | 2.29 | 3.26 | 3.16 |
| 18:00 | 3132 | La Serena vs Coquimbo | 2.20 | 3.12 | 3.07 |
| 18:00 | 3193 | Remo Stars vs Katsina United FC | 1.22 | 5.02 | 12.56 |
| 18:00 | 3221 | Wigan vs Sunderland | 1.95 | 3.38 | 3.68 |
| 18:00 | 3307 | Dundee FC vs Livingston | 2.81 | 3.11 | 2.52 |
| 18:00 | 3978 | St Mirren vs Hearts | 3.11 | 3.16 | 2.29 |
| 18:00 | 4203 | AFC Wimbledon vs Doncaster | 1.71 | 3.68 | 4.51 |
| 18:00 | 4550 | Crystal Palace vs Burnley | 1.91 | 3.41 | 4.11 |
| 18:00 | 4736 | Coventry vs Preston | 1.95 | 3.30 | 3.79 |
| 18:00 | 4881 | Morecambe vs Ipswich | 3.67 | 3.43 | 1.94 |
| 18:00 | 5250 | Brentford vs Newcastle | 2.47 | 3.21 | 2.91 |
| 18:00 | 5475 | Rivers United FC vs Nasarawa United | 1.21 | 5.41 | 11.58 |
| 18:00 | 5736 | Millwall vs Sheffield Utd | 3.25 | 3.20 | 2.18 |
| 18:15 | 3854 | Asteras Tripolis vs Aris Salonica | 2.47 | 2.91 | 3.06 |
| 18:15 | 4045 | Union Saint Gilloise vs Eupen | 1.31 | 5.32 | 8.08 |
| 18:30 | 3879 | Hapoel Hadera vs Maccabi Petach Tikva | 2.54 | 3.06 | 2.63 |
| 19:00 | 3841 | KMC vs Polisi Tanzania | 2.11 | 2.75 | 3.81 |
| 20:00 | 5294 | Empoli vs Juventus | 4.59 | 3.82 | 1.72 |
| 20:30 | 5362 | Everton vs Manchester City | 8.76 | 5.29 | 1.32 |
| 21:00 | 1723 | Hapoel Haifa vs Maccabi Haifa | 6.74 | 4.24 | 1.40 |
| 21:30 | 4227 | Rapid Bucuresti vs Dinamo Bucuresti | 1.91 | 3.33 | 3.91 |
| 22:30 | 3162 | GKS Jastrzebie Zdroj vs LKS Lodz Pss | 4.05 | 3.52 | 1.76 |
| 22:45 | 5509 | Sassuolo vs Fiorentina | 2.70 | 3.55 | 2.46 |
| 23:30 | 1542 | FC Arouca vs Moreirense | 2.22 | 3.20 | 3.20 |
| 23:30 | 2041 | Ayacucho vs Univ San Martin | 1.48 | 4.02 | 5.75 |
| 23:30 | 5236 | Columbus Crew vs Vancouver Whitecaps | 1.63 | 3.81 | 5.41 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KILI MARATHON YATANGAZA BARABARA ZITAKAZOFUNGWA

**Na Dennis Fusi**

ILI kuruhusu mbio za Kilimanjaro Marathon mwaka huu kufanyika kwa ufanisi na usalama, baadhi ya barabara ndani ya Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro zinatarajiwa kufungwa hapo kesho, imeelezwa.

Uamuzi wa kufunga barabara hizo unalenga kuhakikisha usalama kwa washiriki wote.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana inasema uamuzi wa kufunga baadhi ya barabara hizo ni kutokana na ukweli washiriki watatumia njia hizo ikiwamo barabara kuu na madereva watatakiwa kutumia njia mbadala zilizoko maeneo mengine katika manispaa hiyo na pembezoni mwake ili kuepusha usumbufu kwa wakimbiaji.

Katika ufafanuzi wake, taarifa hiyo imeeleza magari yatakayotokea Jiji la Arusha itabidi yasimamishwe kwa muda katika maeneo ya mzunguko wa Arusha na ule ulio eneo la YMCA kwa muda mfupi ili kupisha wakimbiaji kuvuka barabara katika maeneo hayo.

Hatua hii pia itawaathiri madereva wa magari kutoka Dar es Salaam, Marangu na Himo, ambapo washiriki wa mbio hizo wanapaswa wameondoka kwenye barabara hizo ifikapo saa 3:00 asubuhi.

Kwa yale yanayotokea eneo la Machame Wilaya ya Hai hadi barabara ya Sokoine, barabara hiyo itafungwa katika eneo la Shanty Town saa 12 asubuhi sambamba na ile ya mchepuko kwenye Barabara ya Lema.

Barabara ya kutoka Rau hadi Moshi Mjini, itafungwa kuanzia saa moja hadi saa tatu asubuhi ili kutoa nafasi kwa ajili ya mbio za kujifurahisha za kilomita tano.

"Barabara kati ya Masoka hadi Mweka pia itafungwa kati ya saa moja hadi saa tatu asubuhi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Waandaaji hao pia walitangaza maeneo mawili ya kukaa washiriki wa mbio hizo ambayo walisema ni pamoja na eneo la Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) upande wa Mashariki, eneo ambalo hufikika kwa urahisi kwa kupitia barabara ya Uru hadi katika viwanja vya MoCU na pia katika viwanja vya Shule ya Polisi Moshi vinavyoweza kufikiwa kwa kupitia barabara ya Kilimanjaro.

Aidha taarifa hiyo imeeleza ya kuwa kutakuwa na maeneo mawili ya kuegesha magari, yakiwemo magari madogo na mabasi.

"Hakutakuwa na njia ya kuingia MoCU kutoka Barabara ya Sokoine kuanzia saa 12 asubuhi, hivyo wale wote ambao watakuwa na nia ya kuitumia barabara watalazimika kushuka kwenye kona kati ya barabara ya Sokoine na ile ya Kilimanjaro," walisema waandaaji.

Wadhamini wa mashindano haya ambayo yanaingia mwaka wake wa 20 tangu kuanzishwa kwake ni pamoja na Bia ya Kilimanjaro, Tigo na Grand Malt.

Wadhamini wa meza za maji ni pamoja Absa Tanzania, Unilever Tanzania, TPC Sugar, Simba Cement, Kilimanjaro Water; wafadhili wengine ni pamoja na GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel, Surveyed Plots Company Ltd, Bodi ya Utalii Tanzania na CMC Automobiles.



Daktari wa Yanga Princess, Mariam Said (kulia), akimhudumia golikipa wa Ilala Queens baada ya kuumia katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru Jumanne iliyopita. Yanga Princess ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# KMC, Polisi majaribuni Bara

**Na Saada Akida**

LIGI Kuu Tanzania Bara inatarajia kuendelea leo kwa KMC FC kuwakaribisha Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamazi jijini Dar es Salaam.

KMC FC itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kichapo cha mabao 2-0 kutoka kwa Polisi Tanzania walichopata katika mechi ya mzunguko wa kwanza.

Katika mchezo huo KMC FC itawakosa wachezaji wao watatu ambao ni Jean Mugiraneza, Farouk Shikalo na Kelvin Kijiri kutokana na kuwa majeruhi huku Polisi Tanzania ikimkosa Adam Adam ambaye ana matatizo ya kifamilia.

Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kuendeleza ubabe dhidi ya KMC FC kwa kuondoka na pointi tatu muhimu.

"Tunawaheshimu KMC FC, sio wabaya licha ya kwanza kupafa ushindi nyumbani lakini pia tunahitaji kuendelea kupata matokeo mazuri katika mchezo huu wa kesho (leo)," alisema Mketo.

Naye Kocha Msaidizi wa KMC FC, Ahmad Ally, alisema wamejiandaa vizuri na watacheza kwa kuwaheshimu wapinzani wao kwa sababu mechi ya kwanza walipoteza.

# Michezo

Jumamosi Februari 26, 2022

Nipashe






## Dybala anukia kutua England



Mshambuliaji wa Simba, Meddy Kagere (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya beki wa timu hiyo, Joash Onyango wakati wa mazoezi ya kujiandaa na mechi ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya RS Berkane itakayochezwa kesho nchini Morocco. **PICHA: SIMBA SC**

# SIMBA YAANDAA 'SAPRAIZI'

## ●●●Kocha wa RS Berkane asema anawahofia Sakho, Morrison lakini...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI Kocha Mkuu wa RS Berkane, Florent Ibenge, akiwataja nyota anaowahofia ni viungo washambuliaji wa Pape Ousmane Sakho na Bernard Morrison, kikosi cha Simba kilitarajiwa kutua katika mji wa Berkane jana usiku tayari kwa mchezo wake wa Kombe la Shirikisho dhidi ya wenyeji RS Berkane utakaochezwa kesho usiku.

Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, aliliambia gazeti hili jana wachezaji wote wanaendelea vizuri isipokuwa, Jonas mkude hali yake bado haijakaa sawa ingawa juzi alifanya mazoezi mepesi.

"Wachezaji wetu wanaendelea vizuri na Jonas Mkude jana (juzi), alifanya mazoezi lakini leo (jana), nimeona hali yake imebadilika hivyo sina uhakika kama atacheza Jumapili," alisema Rweyemamu.

Meneja huyo aliongeza wametumia muda wa siku tatu kufanya mazoezi nchini Morocco ambayo yamewaongezea nguvu kuelekea mchezo wa kesho na kilichobakia ni mazoezi ya mwisho ambayo watayafanyia kwenye uwanja ambao watautumia kwa mechi hiyo ya Kundi D.

Aliongeza hali ya hewa ya Morocco ni baridi kali hasa nyakati za usiku ingawa tayari wameanza kuizoea lakini ameomba Watanzania wasiache kuwaombea dua njema kuelekea mchezo huo unaosubiriwa na wadau mbalimbali wa soka barani Afrika.

"Tupo vizuri kuelekea katika mchezo wetu wa Jumapili, tunaomba pia Watanzania waendelee kutuombea dua kwa ajili ya kutimiza malengo yetu, tunajua tumebeba bendera ya Taifa, hivyo tutapambana kuhakikisha hatuwaangushi," alisema Rweyemamu.

Aliongeza wanafahamu RS Berkane watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-1 walioupata katika mechi ya Ligi Kuu ya Morocco dhidi ya FAR Rabat iliyochezwa juzi nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ibenge alisema kikosi chake kina mapungufu hasa katika safu ya ulinzi na katika kuhakikisha wanakuwa salama, watalazimika kuwachunga Sakho na Morrison, ambao wameonekana ndio hatari zaidi.

Ibenge alisema amewafuatilia mechi nyingi za Simba ikiwamo michezo miwili ya kimataifa na kubaini nyota hao wamekuwa hatari kwa wapinzani na wamesaidia timu yao kupata matokeo mazuri.

"Kutokana na makosa yanayofanywa na mabeki zangu, tunatakiwa kuwa makini kuwachunga wachezaji wote wa Simba, wakiwamo Sakho na Morrison ambao wamekuwa hatari sana katika kuisaidia timu hiyo,".

"Simba ni timu kubwa, tunakabiliwa na mchezo mgumu dhidi yao, ukiangalia mechi zao mbili kuna watu ambao kama wanataka kushinda lazima watafute mbinu za kuwatuliza," alisema kocha huyo.

Alisema amemwona Sakho akicheza ni mchezji mwepesi anayehitajika kuangaliwa sana kwa jinsi alivyoona na pamoja na taarifa zake alizopata kupitia mechi zao za hivi karibuni.

"Kuna yule Morrison ni mzuri mwenye ubora akiwa uwanjani achilia mbali nidhamu yake, namjua vyema ni lazima tuwe na umakini na akili ya kuwazuia," alisema Ibenge.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Steven Mnguto, amewataka Watanzania kuungana pamoja kuiombea Simba kwa sababu wamefanya kazi kubwa mpaka hapo walipofika.

"Ninaomba Watanzania tuungane pamoja tuiombee timu yetu ambayo imepambana mpaka ikafanikiwa kufika hapo," alisema Mnguto.

# Yanga yashikilia rekodi safi Bara

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara Jumatano iliyopita, Yanga imeweka rekodi nyingi nzuri, mbali na kuongoza, kufunga mabao mengi, kufungwa magoli machache, ikiwa haijapoteza mechi yoyote, lakini pia ndiyo timu iliyovuna pointi nyingi ikicheza ugenini.

Kwa mujibu wa rekodi zilizotolewa na Bodi ya Ligi mara baada ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, Yanga pia ndiyo timu iliyocheza faulo chache zaidi kuliko klabu nyingine nyingine ile kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hadi kumalizika kwa mzunguko huo.

Rekodi zinaonyesha Yanga inaongoza Ligi Kuu ikiwa na pointi 39, imeshinda mechi nyingi zaidi kuliko timu yoyote ambazo ni 12, huku ikiwa ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mchezo wowote hadi mzunguko huo wa awali unamalizika.

Mbali na rekodi hiyo, Yanga pia imevuna pointi 23 ikicheza ugenini ambazo ni nyingi zaidi kuliko timu yoyote ile.

Imecheza mechi tisa ugenini, ikishinda saba na kutoka sare mbili, ikifuatiwa na Simba ambayo imecheza mechi saba za ugenini, ikishinda tatu, sare mbili na kupoteza mechi mbili, ikivuna pointi 11 ugenini, huku timu za Kagera Sugar na Namungo zikipata pointi 10 ugenini kila moja.

Takwimu hizo pia zinaonyesha pia Geita Gold, Tanzania Prisons na Mtibwa Sugar, zimevuna pointi chache zaidi, kwani kila moja imepata pointi tano tu ikicheza nje ya uwanja wake wa nyumbani.

Yanga pia ndio timu iliyocheza faulo chache zaidi kwenye mzunguko wa kwanza, ikicheza madhambi mara 118, ikifuatiwa na Simba ambayo imecheza madhambi mara 156 lakini pia vinara hao ni moja kati ya timu sita, ambazo hazijazawadiwa kadi nyekundu mpaka sasa, nyingine ni Azam FC, Prisons, Geita Gold, na Biashara United.

Mshambuliaji wa Namungo, Reliants Lusajo yeye ameipaisha timu yake kwa kuwa ndiye mfungaji mwenye mabao mengi, amepachika wavuni magoli 10 na anafuatiwa na George Mpole wa Geita Gold na Fiston Mayele wa Yanga, wenye mabao saba kila mmoja.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042